

Pambazuko

Toleo Namba 186

Jumatatu, Oktoba 12-18, 2026

Freeman Mbowe ni konokono na mwanzi wa kisiasa Uk. 20

Hifadhi ya barabara sasa yapangishwa

Moja ya bar inayojengwa kwenye hifadhi ya barabara ya Morogoro eneo la Kibanda cha Mkaa, Mbezi jijini Dar es Salaam.

Habari Uk. 6&7



Jicho la Tai

Nani katuroga hata tunakaribia kusahau kuna mwanga na giza!

INAFURAHISHA sana kuishi kwenye nchi ambayo ukienda kulala, unalalia kitanda chenye godoro lililonakshiwa kwa tanzanite na shuka lenye upindo uliofumwa kwa vipande vidogo vya dhahabu.



Safu Uk. 5


Watanzania wakwama kuwekeza Dangote

Habari Uk. 9



Nyerere angeuliza maendeleo haya yanamlinda nani?

Uk. 14



Hali ni mbayaaa! ● Kisukari tishio la maisha Tanzania

Uk. 12

■ Tahariri

Polisi wasimamie sheria, walinde maisha barabarani

KILA kilio kinachosikika baada ya ajali ya barabarani kinatukumbusha wajibu ambao taifa haliwezi kuendelea kuupuuza.

Nyuma ya taarifa za vifo na majeruhi kuna familia zinazopoteza watoto, wazazi na nguvu kazi ya taifa. Mbali na vifo, kuna ulemavu na uharibifu wa mali na miundombinu.

Kimsingi, hatupaswi kuzoea maafa haya kana kwamba ni gharama ya kawaida ya kusafiri.

Pambazuko inaitaka serikali, kupitia Jeshi la Polisi, kuimarisha usimamizi wa sheria za barabarani kwa uthabiti, weledi na bila upendeleo.

Dereva anayehatarisha maisha kwa mwendo usio salama, kupita magari kiholela au kupuuza masharti ya usalama lazima awajibishwe. Umarufu wa kampuni, utajiri wa mmiliki au uhusiano wake na viongozi visiwe kinga dhidi ya sheria.

Ukali tunaoutaka ni wa utekelezaji wa sheria unaozingatia haki na ushahidi. Hatuhimizi udhalilishaji, matumizi ya nguvu yasiyo lazima wala adhabu zinazotolewa kwa hasira.

Pambazuko tunataka hatua halali, zinazofuatiliwa na kuleta mabadiliko ya tabia. Tunatambua kwamba onyo lisilofuatiwa na uwajibikaji, linaweza kumjengea mkosaji mazoea ya kudharau mamlaka.

Pamoja na kutambua umuhimu wa ushirikiano kati ya polisi na watoa huduma za usafiri, lakini uhusiano huo unapozidi, unaweza kujenga ushirika wa kishetani unaofumbia macho kufuatwa kwa sheria za barabarani, hivyo kuwa chanzo cha ajali nyingi tunazoshuhudia sasa.

Pambazuko haipingi ukaribu wenye afya un-aosaidia elimu, mawasiliano na utekelezaji wa sheria, lakini urafiki unapofifisha mipaka ya kazi, wananchi wana sababu ya kuhoji iwapo usalama wao unapewa uzito unaostahili.

Ukaribu wa askari wa barabarani au maofisa wakubwa na wenye kampuni za mabasi haupaswi

kuathiri uamuzi wa kitaaluma na haki.

Pale panapojitokeza viashiria vya upendeleo, malalamiko yachunguzwe kwa uwazi.

Malalamiko dhidi ya wanaolegeza sheria, kufumbia macho makosa au kuwalinda wakosaji yashughulikiwe bila kulindana.

Nidhamu ya ndani ni msingi wa mamlaka ya polisi kudai nidhamu kutoka kwa madereva.

Wamiliki wa mabasi nao wana wajibu mkubwa, lazima wazingatie ratiba zinazoweza salama madereva wao pamoja na abiria.

Gari salama, dereva mwenye uwezo na muda wa kupumzika ni sehemu ya wajibu wa biashara, siyo hisani kwa abiria.

Wananchi pia wasiwe watazamaji wa hatari inayowakabili. Dereva anapoendesha kwa fujo, abiria waombe kwa uthabiti apunguze mwendo na azingatie sheria.

Abiria wasimshangilie kwa kuwahi kufika huku akiwaweka katika hatari. Ukimya wa abiria unaweza kumpa dereva hisia kwamba mwenendo wake unakubalika.

Hata hivyo, abiria wasimvamie dereva, kumshika au kuanzisha vurugu zinazoweza kuongeza hatari.

Watoe taarifa kwa polisi na kampuni ya usafiri kwa namna salama, wakieleza namba ya gari, eneo na kosa lililoonekana.

Tunataka pia ukaguzi wa magari na ufuatiliaji wa makosa uwe endelevu, badala ya kusubiri msiba ndipo operesheni zianze.

Taarifa za wananchi zitumike kubaini maeneo yenye hatari na madereva wanaorudia makosa. Mafanikio yapimwe kwa usalama unaoongezeka, siyo wingi wa faini pekee au matangazo ya kukamata magari.

Maisha ya wananchi yana thamani kuliko faini, urafiki au faida ya safari. Polisi wakisimamia sheria bila upendeleo, wamiliki wakitimiza wajibu na abiria wakikataa uzembe, tunaweza kupunguza maafa.

Barabara zetu ziwe njia za kufikisha watu salama, badala ya kuendeleza vilio vya familia na kupoteza nguvu kazi za taifa letu.

Zima moto kazini... ■



Askari wa Kikosi cha Zimamoto Mkoa wa Morogoro wakiwa eneo la Mkambarani baada ya kuzima moto wa ajali ya lori na basi la abiria iliyosababisha vifo vya watu wanaofikia 32 na majeruhi mwishoni mwa wiki. (Na Mpi-gapicha Wetu)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

■ Dunia: Hapa na Pale

Trump akasirika kukosa Nobel

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameonyesha hasira zake hadharani baada ya kukosa Tuzo ya Amani ya Nobel, akieleza kutoridhishwa kwake na uamuzi wa kamati ya tuzo hiyo na kwamba uteuzi wa mwaka huu kuwa “aibu na fedheha.”

Amekosoa zaidi akisema kuwa hajawahi hata kumsikia mshindi aliyetangazwa kushinda tuzo hiyo kwa mwaka huu. Mshindi aliyetangazwa ni jaji wa zamani wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai, Navi Pillay, aliyetangazwa rasmi Ijumaa iliyopita.

Trump amekuwa akieleza mara kwa mara kwamba anaamini anastahili kutunukiwa tuzo hiyo na hii siyo mara ya kwanza kulalamikia uamuzi wa kamati hiyo, ambapo mwaka 2025 pia alikosoa tuzo hiyo baada ya kutolewa kwa kiongozi wa upinzani wa Venezuela, María Corina Machado.

Amesema uamuzi huo ni doa kwa Norway na akaonya kwamba hatua hiyo haitasahaulika kirahisi. Mwaka jana wakati Trump analalama, Waziri Mkuu wa Norway, Jonas Gahr Støre, alimkumbusha kwamba mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel huchaguliwa na kamati yake huru yenye makao yake nchini Norway, na siyo serikali ya nchi hiyo.

Sasa kunyongwa hadharani

MAREKANI imerejesha utekelezaji wa kunyonga watu waliohukumiwa kifo kwa kunyongwa hadharani na tayari maelfu ya watu wameshuhudia tukio moja lililofanyika kandokando ya mto mji-ni Owensboro, katika jimbo la Kentucky.

Katika tukio hilo, mwanamume mweusi aliyepatikana na hatia ya kumbaka na kumuua mjane wa kizungu mwenye umri wa miaka 70, alinyongwa hadi kufa hadharani.

Baadhi ya watu walikesha karibu na jukwaa la kunyongwa ili kupata nafasi nzuri ya kushuhudia tukio hilo, huku wengine wakifanya sherehe usiku uliotangulia, huku baadhi ya vijana wakizunguka wakiuza bisi na vinywaji kwa umati wa watazamaji.

Mahakama yampoka gari

MWALIMU Evans Sichei wa Nairobi, Kenya amepoteza gari lake la thamani ya Shilingi milioni 1.7 baada ya Jaji B.M. Musyoki wa Mahakama Kuu kuamua kuwa gari hilo litwaliwe na serikali kwa kuwa mwalimu huyo hakueleza vizuri alikopata fedha za kulinunua.

Ilidaiwa kwamba ununuzi wa gari hili huenda ulitokana na kujihusisha na biashara ya ulanguzi wa watu kinyume cha sheria.

Mahakama ilisema Mamlaka ya Kurejesha Mali (ARA) ilionyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa gari hilo lilinunuliwa kwa mapato ya uhalifu.

Kesi hiyo ilitokana na uchunguzi kuhusu madai ya Wakenya kusafirishwa hadi Thailand kwa ahadi za ajira zenye mishahara mizuri, lakini baadaye kupelekwa Myanmar ambako walilazimishwa kufanya uhalifu wa kimtandao katika mazingira magumu.



Wahubiri waizidi nguvu serikali

SERIKALI ya Ghana imesitisha kwa muda utekelezaji wa marufuku ya kuhubiri ndani ya mabasi na vyombo vingine vya usafiri wa umma vinapokuwa katika mwendo, kutokana na wasiwasi ulioibuliwa na viongozi wa dini na waumini.

Kanuni mpya za usalama barabarani zilikuwa zimezuia kuhubiri na kufanya biashara ndani ya vyombo vya usafiri wa umma vinapokuwa safari-ni, huku wanaokiuka sheria hiyo wakikabiliwa na kifungo au faini.

Msemaji wa serikali, Felix Kwakye Ofosu (pichani), amesema utekelezaji wa kanuni hiyo umesitishwa ili kutoa nafasi kwa mashauriano zaidi na wadau wa kidini.

Nchini Ghana, ambako Wakristo ni wengi, mahubiri ndani ya mabasi ni jambo la kawaida na limekuwa sehemu ya maisha ya kila siku kwa miaka mingi.



Nani katuroga hata tunakaribia kusahau kuna mwanga na giza!

INAFURAHISHA sana kuishi kwenye nchi ambayo ukienda kulala, unalalia kitanda chenye godoro lililonakshiwa kwa tanzanite na shuka lenye upindo uliofumwa kwa vipande vidogo vya dhahabu.

Hata hivyo, pamoja na kupata usingizi juu ya utajiri huo, ukiamka asubuhi unakunywa uji wa muhogo usio na sukari kwa sababu huna mia mbili ya kiberiti.

Nchi yangu ina miujiza ya kipekee duniani; nchi pekee ambapo madini ya nadra hayapatikani popote kuanzia Tokyo hadi New York, lakini wanchi wake walioko mita chache kutoka machimbo hayo bado wanaomba msaada wa vyandarua vyenye dawa kutoka kwa wafadhili.

Hivi kweli tumerogwa, au huyu mganga aliye-turoga alikufa na ufunguo wa akili zetu?

Wakati mwingine akili yangu inasema kudhani kwamba tumerogwa ni kuwasingizia bure wachawi, lakini ukweli mchungu uliopo, na unaouma zaidi, ni kwamba hatujarogwa na mtu yeyote kutoka nje; tumeamua kujiroga wenyewe kwa kuwafuga “mchwa” wa kisasa wenye suti na tai.

Mchwa hawa hawali mbao tena; wamehamia kwenye karatasi za mikataba na akaunti za benki. Wana uwezo wa ajabu wa kuhomola kila senti inayotokana na jasho la madini yetu na kuihamishia kwenye akaunti za siri kule Dubai, Uswisi na Visiwa vya Jersey, ambako wanaficha fedha walizochuma kutoka hapahapa.

Kutokana na mchwa hawa kuenea kila mahali, nimepata wasiwasi endapo yale yaliyomo kwenye Dira ya Maendeleo ya 2050 yatafikiwa.

Nimesoma na kutafakari yaliyomo kwenye dira hiyo. Hakika ni waraka mzuri sana, ulioandikwa kwa lugha yenye maneno ya kuvutia yaliyosheheni namba na chati za kupendeza, lakini napata shida kidogo na kujiuliza; “katika mazingira haya ambapo mchwa wanaendelea kutafuna, dira hii itafikiwa kweli?”

Au nayo itafuata nyayo za dira zilizopita na kwenda kupumzika kwa amani kwenye makabati, ikisubiri kufutwa vumbi na vizazi vijavyo vina-
vyokuja kushangaa jinsi babu zao walivyokuwa



mabingwa wa kupanga lakini wazito wa kutenda?

Kama tunataka dira hii isigeuke kuwa hadithi ya Alf Lela Ulela, ni lazima tuchukue hatua za makusudi na za busara kuliko maneno tupu na yafuatayo yafanyike.

Lazima tutengeneze viutilifu vikali vya kisheria na kiuwajibikaji ili kuwateketeza mchwa hawa waliojificha ndani ya mifumo yetu. Haku-na maendeleo yatakayofika ikiwa kila shilingi ya madini na kodi inaishia mifukoni mwa watu wachache wanaoshindana kwa ukwasi.

Kwamba wakati umefika sasa kuacha mikataba ya kificho inayofanywa gizani. Kila tone la madini linalotoka katika ardhi yetu lazima lilete shule bora, hospitali zenye dawa, na barabara za kisasa, na siyo sifa zisizoweza kuimarisha maendeleo ya kila kaya.

Ni muhimu sasa kuhimiza ujenzi wa viwanda vya ndani ili kuchakata madini yetu badala ya kusafirisha udongo na madini ghafi nje ya nchi. Ni lazima sasa tuchongee na kusafisha madini yetu hapa nyumbani ili kutengeneza ajira za kweli kwa vijana wetu.

Ni muda wa kuamka sasa kutoka kwenye usingizi huu wa pono. Hatuwezi kuendelea kuwa walinzi wa utajiri wa dunia huku wenyewe tukitembea vifua wazi na kukabwa kwa njaa.

Historia mpya lazima iandikwe sasa na kuke-me laana ambayo inaweza kutufika kwa baadhi yetu kuendelea kuhomola rasilimali zetu kwa manufaa binafsi.

■ Habari Kuu

Hifadhi ya barabara yapangishwa



Malori yakiwa yameegeshwa karibu na Stendi ya Daladala Mbezi ambayo imekondishwa kwa wamiliki wa malori.

Na Waandishi WETU

SEHEMU ya eneo la Hifadhi ya Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam - kutoka Kimara Stop Over hadi Kiluvya, limepangishwa na sasa ujenzi unaendelea kwa kasi, Pambazuko limebaini.

Eneo hilo liko chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads).

Hilo ni eneo ambalo hadi mwaka 2016 lili kuwa na majengo ya biashara na makazi, na kuvunjwa bila kulipwa fidia.

Sasa maendeleo ya ujenzi wa vituo vya mafuta na hoteli, kumeibua maswali lukuki kuhusu upangishwaji wa eneo hilo.

Timu ya Pambazuko imefanya ufuatiliaji wa kina kujua kinachoendelea katika maeneo hayo, ambapo kiongozi wa kundi la wananchi 160 waliovunjiwa nyumba za makazi na majengo ya biashara katika maeneo hayo awali, Chritian Kibogoyo amesema uwekezaji unaoendelea una ukakasi kwa kuwa hauangalii namna ya kuwasaidia wao wakiwa waathirika.

Amesema kama Tanroads wameamua kupangisha wawekezaji baada ya kuwanyang'anya maeneo yao kwa kisingizio cha hifadhi ya barabara, kwa nini hawakuwaambia waingie ubia na wafanyabiashara hao?

Amesema wameamua kuendelea na kesi iliyoko Mahakama ya Ardhi na zaidi wamepata nguvu baada ya kuona kasi ya upangishaji huo wa maeneo kuwa ushahidi wa wazi kwamba kwa nini waliwatoa kwa kisingizio cha hifadhi ya barabara!

“Kinachofanyika ni kumtia mnyonge umasikini na kumwinua tajiri, jambo ambalo linaonyesha kulikuwa na uonevu ili baadaye waje kuweka majengo, vituo vya mafuta, hata sisi tungeweza kuweka hivyo vituo kwa kuingia ubia na wawekezaji...”

“Miongoni mwetu tuliovunjiwa na serikali wakati wa utawala wa Rais John Magufuli kwa kisingizio cha hifadhi ya barabara, kumbe wali-tuonea tu,” anasema Kibogoyo.

Akaendelea; “Basi kama wangukuwa waungwana wakatulipa fidia, hata leo waamue waje tukae tujadiliane, watulipe fidia. Hakuna mtu anayeweza kuzuia maendeleo, wote tunataka barabara nzuri, lakini siyo kutudhulumu,” amesisitiza.

Gharama za upangishaji

Chanzo cha kuaminika kutoka eneo hilo, kimeleleza Pambazuko kuwa gharama za upangishaji katika maeneo hayo ni wastani wa dola 5 za Marekani (karibu Shilingi 13,500) kwa mita moja ya mraba na malipo yake yanalipwa kwa mwaka mzima.

Kwa mujibu wa vyanzo hivyo vya taarifa, kituo kidogo cha mafuta chenye pampu tatu kinatikiwa kuwa na wastani wa mita za mraba 2000, hivyo kwa mita za mraba 2000 – ikiwa kweli ndiyo eneo stahiki, malipo yake yanaweza kufikia zaidi ya Shilingi milioni 26 kwa mwaka.

Inaendelea Uk. 7

Hifadhi ya barabara

Inatoka Uk. 6

Aidha, kituo kikubwa ni kile chenye pampu sita na kuendelea, kinaweza kuwa na mita za mraba 4000, hivyo malipo ya mwekezaji kwa mwaka yanaweza kufikia wastani wa zaidi ya Shilingi milioni 52.

Hifadhi ya barabara

Hifadhi ya barabara ni eneo au kipande cha ardhi kilichotengwa au kuhifadhiwa kwa ajili ya maendeleo na upanuzi wa barabara au shughuli zingine zinazohusiana na mambo ya barabara.

Eneo hili la barabara, linatambulika kisheria, na sheria zinazotambua hifadhi ya barabara ni kama zifuatavyo:

Kifungu cha 6 (1) (vii) cha Sheria ya Ardhi, sura ya 113 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019. Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007, pamoja na kanuni zake za mwaka 2009.

Sheria ya hifadhi ya barabara inasemaje?

Sheria ya barabara ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009, kifungu cha 29 (2) na (3) cha Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009, zinai-pa Tanroads mamlaka ya kutoa kibali cha muda mfupi kwa mtu yoyote anayehitaji kutumia eneo la hifadhi ya barabara kwa matumizi yali-yoruhusiwa, na pia matumizi yake, hayata athiri upanuzi au matengenezo ya barabara pindi ya-takapo hitajika.

Kwa siku mbili mfululizo, Pambazuko lil-imtafuta Meneja wa Tanroads Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi Alinanuswe Kyamba kwa ajili ya kupata ufafanuzi kuhusu utaratibu unaotu-mika katika uendelezaji wa maeneo hayo ya hi-fadhi ya barabara, lakini halikufanikiwa kupata ushirikiano wa kutosha.

Ijumaa, Oktoba 9, 2026 Pambazuko lilifika Ofisi za Tanroads Mkoa wa Dar es Salaam – saa 4:17 asubuhi, lakini lilishindwa kuonana na uongozi kwa maelezo kuwa wote walikuwa kati-ka shughuli nyingine nje ya ofisi.



Ujenzi wa kituo cha mafuta ukiendelea katika hifadhi ya Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Temboni, Dar es Salaam.

Hata baada ya kumpata kupitia simu yake ya mkononi saa 6.38 ya mchana wa Jumamosi - Oktoba 10, 2026 alimtaka mwandishi amsubiri kwa muda akisema atampigia, kwa kuwa aliku-wa na jukumu la kumalizia kwa wakati huo.

Saa tatu baadaye, majira ya saa 9.43 alasiri mwandishi alimtafuta tena kwa simu na alipo-pokea alimwambia; “Nimekwambia subiri, nita-kupigia” kisha akakata simu.

Jioni ya Juamamosi, alipotafutwa tena – saa 10:21, aliahidi kutoa ufafanuzi na maelezo ya kina leo - Jumatatu Oktoba 12, 2026.

Awali, Pambazuko lilizungumza na mmo-ja wa maofisa wa Tanroads, na kueleza kuwa mamlaka hiyo haijawahi kutoa ruhusa kwa watu kujenga kwenye hifadhi ya barabara.

Kiongozi huyo ambaye alikataa jina lake kuandikwa gazetini alisema kila mtu anawajibi-ka kutafuta taarifa kutoka mamlaka mbalimbali ikiwamo Tanroads, kujua uhalali wa eneo analo-taka kununua au kujenga kabla ya kuanza ujenzi ili aepuke kuvunjiwa.

“Barabara nyingi hasa za mijini zimewekwa mawe ya alama ya hifadhi kati ya mita 100 na 200, lakini baadhi ya watu wanazing’oa au kuz-iziba makusudi. Tunawaasa wananchi wote ku-fuata sheria bila shuruti”.

■ Habari Kuu



Kituo cha mafuta Kimara Temboni kilichopo katika hifadhi ya Barabara ya Morogoro.

Hifadhi ya barabara

Inatoka Uk. 7

Eneo la hifadhi

Kwa mujibu wa taarifa za Tanroads zinazopatikana katika tovuti yake, Barabara ya Morogoro, katika eneo la Ubungo, Dar es Salaam hadi Kibaha, Pwani inalindwa na Sheria ya Hifadhi ya Barabara ya Mwaka 1932 na mipango ya serikali.

Sheria hiyo inataja umbali tofauti wa hifadhi ya barabara katika baadhi ya maeneo na imeendelea kuwa mwongozo kwa barabara hiyo ya Morogoro.

Tanroads wameainisha kuwa upana wa Hifadhi ya Barabara ya Morogoro unatofautiana kulingana na maeneo na umbali kutoka Sanamu ya Askari, Dar es Salaam, ukiwa kati ya mita 60 hadi 120 kwa jumla.

Wameainisha viwango vya hifadhi barabara ya Morogoro kuwa ni katika kilometa 0 hadi 10: Upana wa jumla ni mita 60 – Faya hadi Ubungo (mita 30 kila upande kutoka katikati), kilometa 10 hadi 16: Upana wa jumla ni mita 90 – Ubungo hadi Kimara Stop Over (mita 45 kila upande

kutoka katikati) na kilometa 16 hadi 37 (kama vile maeneo ya Kimara-Stop Over hadi Kiluvya-Kibaha).

Kutokana na sheria hiyo, ndiyo maana zipo nyumba zilizokuwa kati ya Ubungo na Kimara ndani ya mita 90 kutoka katikati ya barabara, zilibomolewa - kutoka Kimara Stop Over hadi Kiluvya ziko ndani ya mita 121.9.

Ubomoaji huo ulianza kutekelezwa mwaka 2017 ili kupisha ujenzi wa barabara ya njia nane kuanzia Kimara/Ubungo hadi Kibaha.

Sheria ilibadilishwa katika maeneo mengine mwaka 1967 na baadaye mwaka 2000, lakini katika Hifadhi ya Barabara ya Morogoro haijawahi kubadilishwa. Sababu mojawapo ni kwamba hii ni barabara kuu hapa nchini.



Ujenzi wa kituo cha mafuta Kimara Temboni

Watanzania wakwama kumiliki Dangote

Na Mwandishi WETU

WATANZANIA wengi waliokuwa wanatamani kununua hisa za kampuni ya kusafisha mafuta ya Dangote nchini Nigeria, wamekwama kutimiza ndoto zao.

Pambazuko limebaini kuwepo kwa mkwamo huo katika zoezi la kuuza hisa za Dangote ambalo linafungwa kesho, Oktoba 13. Uuzaji wa hisa hizo ulifunguliwa Septemba 14, 2026.

Changamoto inayojitokeza ni tofauti kati ya upatikanaji wa hisa kupitia majukwaa ya kimataifa na uwepo wa utaratibu ulioidhinishwa wa kuzitangaza na kuziua katika kila nchi.

Gazeti la Pambazuko, pamoja na kukosa ushirikiano wa kujua idadi ya Watanzania walioweza kununua hisa hizo, lakini limeelezwa kuwa idadi yao ni ndogo mno.

Mkwamo wa kupata hisa hizo unadokeza kuwepo kwa kuchelewa kupatikana kwa vibali vya mamlaka za masoko ya mitaji, hasa kwa nchi za Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania.

Hali hiyo iliibua maswali kuhusu namna wananchi wa kawaida wanavyoweza kushiriki uwekezaji unaotangazwa kuwa wa Waafrika.

Kwa mujibu wa tovuti rasmi ya mauzo, Dangote Petroleum Refinery and Petrochemicals inatoa hisa za kawaida bilioni 4.1, kwa bei ya dola za Marekani 0.4 kila moja. Bei ya hisa moja ni takribani Shilingi 1,052 (dola 0.4), huku kiwango cha chini cha hisa 10 kikigharimu takribani Shilingi 10,524, kabla ya ada nyingine.

Pambazuko limebaini kuwa njia iliyokuwa rahisi ya kupata hisa hizo ilikuwa kupitia majukwaa maalumu ya kidijitali.

Jukwaa la MyStocks limeeleza kuwa linapokea maombi kutoka Tanzania, baada ya uhakiki wa utambulisho na ustahiki wa akaunti.

Katika mfumo huo, hisa hushikiliwa kwa pamoja kwa niaba ya wawekezaji, badala ya kila mnunuzi kuandikishwa moja kwa moja kwenye rejista ya Nigeria.

Wakati Tanzania ikisubiri ufafanuzi wa utaratibu wa ndani, Kenya na Uganda zimechukua hatua za kuruhusu wawekezaji wao kushiriki,



Aliko Dangote

ingawa nao wamedai kuwepo kwa mkwamo wa kufikia hatua ya mwisho ya kulipa na hatimaye kupewa hati ya kutambulika kuwa mwanahisa.

Kiwanda cha Lagos kiligharimu takribani dola bilioni 20 kujengwa, huku thamani yake katika mauzo ya hisa ikikadiriwa kuwa dola bilioni 47.59. Dangote pia anajenga kiwanda kingine cha kusafisha mafuta huko Lamu, Kenya ambao utagharimu dola bilioni 16.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa “waliochan-gamkia” hisa za kampuni za Dangote, ni wafanyabiashara na kampuni kubwa za Marekani na Ulaya.

Kwa Watanzania, suala kuu sasa ni kupata maelezo, kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuhusu vibali, gharama, utunzaji wa hisa na njia halali za malipo kabla ya muda kuisha, ambao ni kesho.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA



Nimewasikia TRC kuhusu SGR

KWANZA napenda kuushukuru uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa kutoa ufa-fanuzi juu ya “swali” langu la Oktoba 7, 2026 ikiwa treni yetu ya mwendokasi (SGR) inahujumiwa au shida ya mtandao?

Nimefurahi kwamba mmefafanua kwa uungwana nami nawapongeza.

Baada ya kukosa ndege, niliingia mtandaoni kutafuta tiketi. Siti zote za Oktoba 7 na siku iliyofuata; Oktoba 8 kwa madaraja yote zilikuwa zimejaa. Ndipo nililazimika kutafuta msaada wa “kujuana” nikapata tiketi.

Kama siti zilikuwa zimeuzwa na abiria ha-wakutokea, basi shirika linatengeneza faida kwa kutosafirisha watu! Nina picha zaidi ya nilizo-onyesha, kwamba siti nyingi hazikuwa na watu mpaka Dodoma.

Nilihojiana na wafanyakazi wawili (msiwatafute kwenye CCTV camera) na walikuwa na

ujasiri kuniambia kwamba, “siti zote za mada-raja ya chini zinafungwa mtandaoni ili abiria waende na mabasi.” Tuhuma hii isipuuze.

Ni kweli nilisafiri na treni ya mwendoka-si isiyo na daraja la uchumi (economy), lakini business class ndiyo economy kwa royal class.

Nilizunguka mabehewa yote na kukuta wafa-nya usafi wanatunza vifaa vyao vyooni na kusa-babisha kero kwa watumiaji.

Napenda kwa moyo wote kuishauri TRC ku-chukulia kwa uzito maoni na ukosoaji wowote bila kinyongo ili kuliepusha shirika na kupor-omoka mapema.

Mimi sikuhukumu, niliuliza swali.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Tumeshindwa wapi mauaji ya wake 150 na waume 11?

KATIKA kipindi cha wiki moja tumepata taarifa za kusikitisha za wanawake watatu waliouawa na wapenzi wao.

Hizi siyo taarifa za kuchukuliwa kama jambo la kawaida kwani ni ukatili unaoendelea tena ukionekana kuongezeka. Je, tumeshindwa wapi?

Tukiangalia uchambuzi wa @waizer_esa kutoka katika taarifa za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kati ya 2019-2023, unaonyesha kuwa katika kipindi hicho wanawake 150 waliuawa na wapenzi wao ikilinganishwa na wanaume 11.

Hizi siyo namba tu, ni maisha ya mwanamke, familia iliyopoteza mama, dada, binti au mke na watoto wakiwa na majeraha yasiyoonekana na uyatima.

Kinachotisha zaidi, mauaji haya hayawezi kuchukuliwa kama matukio yaliyozuka ghafla. Kunakuwepo na viashiria. Ukatili huweza kuanza kwa maneno ya vitisho, wivu uliopitiliza, uhibititi wa mwenz, kutengwa na familia au marafiki, vipigo na aina mbalimbali za unyanyasaji.

Hata jamii inayowazunguka wahuika hufahamu hali inayoendelea ila huwa wanasema; 'Hayo ni mambo ya ndani,' 'yatakwisha tu' 'wanawake wakiaswa wasivunje ndoa.'

Tujiulize iwapo kauli kama hizi zina mchango gani katika yanayokuja kutokea? Je, kuna mifumo gani mahsusi ya ulinzi kwa mwanamke anayejisikia kutishiwa maana hata wanaoamua kuondoka huweza kufuatwa walikokimbilia na kudhuriwa.

Je, upo msaada pale mwanamke anapotoa taarifa za vitisho vinavyofanywa na mpenzi wake? Taarifa hizo huchukuliwa kwa uzito gani na yeyote anayezipokea? Tuendele kujiuliza tunawafundisha nini watoto wetu kuhusu mahusiano?

Mara nyingi, wasichana wanafundishwa kuwa makini na wanaume, wasikubali kunyanyaswa, jambo ambalo ni muhimu kabisa, lakini tumewaelekeza je hao wavulana ambao wasichana wanapaswa kuwa makini nao?

Wavulana wamefundishwa kwamba kumpenda mtu siyo kumiliki maisha ya mtu huyo? Hivi wanafahamu wivu siyo uthibitisho wa upendo? Vilevile wanaelewa kuwa kukataliwa au kudanganywa siyo sa-

babu ya kulipiza kisasi? Na zaidi wanafahamu kuwa migogoro haitatuliwi na vitisho au manguvu?

Kama jamii, hatupaswi kusubiri mwanamke auawe ndipo familia, na mamlaka zichukue hatua. Kwanza, vitisho dhidi ya maisha visichukuliwe kama ugomvi wa kawaida kwa wapenzi.

Anapoinuka mtu na kusema ametishiwa kuuawa, hilo lichukuliwe kwa uzito wake na aweze kupatiwa njia salama ya kupata ulinzi na msaada.

Pili, majirani na familia wasiwe ndugu watazama, tuache kabisa kuona hayo ni mambo yao na siyo yetu.

Tatu, vyombo ya ulinzi viwe na utaratibu wa kutambua na kufuatilia vitisho vinavyoweza kuzaa mauaji.

Nne, pawepo na huduma zinazofikika kwa wanawake walio katika hatari, yaani mahali salama wanapoweza kwenda kujihifadhi.

Isiwepo hali ambayo mwanamke atapaswa kuchagua kati ya kurudi kwa mnyanyasaji au kukosa mahali pa kwenda.

Tano, elimu zaidi ya kuzuia ukatili ianze mapele majumbani, shuleni, kwenye nyumba za ibada. Vijana wafundishwe kuhusu, heshima ya utu, ridhaa, kudhibiti hasira na njia zifaazo kutatua migogoro bila kutumia nguvu.

Mwisho tunahitaji kupata data bora zaidi. Kila mauaji ya mwenz yachambuliwe kwa kina ili kujua iwapo viliwahi kuwepo vitisho, vipigo kabla ya kifo.

Tusipojua tuliposhindiwa si rahisi kujenga kinga itakayofaa. Hawa wanawake watatu waliouawa wiki hii, wasiwe habari nyingine zitakazopita na kusahaulika haraka, bali ziwe sababu ya taifa kujiuliza kwa dhati tujenge mfumo gani kuzuia haya?

Hebu tugeuze takwimu kuwa hatua, hatua kuwa kinga na kinga kuwa maisha yaliyookolewa. Swali lisiwe nani atakayefuata, bali liwe tunafanya nini ili asiwepo namba 151?

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240..

■ Habari

Hali ni mbayaa!



Waziri wa Afya Mohammed Mchengerwa

Na Mwandishi WETU

WAKATI Tanzania ikitajwa kuwa ya pili kwa nchi za ukanda wa Afrika kuwa na wagonjwa wengi wenye kisukari, wataalamu wa afya wameeleza kuwa vinywaji vyenye sukari nyingi, ni sababu ya ongezeko la wagonjwa hao nchini.

Shirikisho la Kimataifa la Ugonjwa wa Kisukari (IDF), linabainisha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi tano za Afrika zenye idadi kubwa ya watu wazima wenye ugonjwa wa kisukari.

Idadi inayokadiriwa ya wagonjwa wa kisukari Tanzania ni milioni 1.9 – kwa takwimu za mwaka 2024. Hawa ni watu wenye umri wa miaka kuanzia 20 hadi 79.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Lucas Mkeni, amesema vinywaji vyenye sukari nyingi, ni sababu ya ongezeko la wagonjwa wa kisukari nchini.

Akizungumza hivi karibuni kupitia Kituo cha Televisheni ya Taifa (TBC), Dkt. Mkeni

amesema kemikali zinazopatikana katika vinywaji na vyakula vya viwandani ambavyo vina sukari nyingi, husababisha uraibu na kuongeza hatari ya magonjwa ya muda mrefu kama kisukari, shinikizo la damu na saratani.

Mtaalamu huyo pia ameonya ulaji au unywaji wa sharubati (juisi) ya matunda mchanganyiko ambayo yana kiwango kikubwa cha sukari (high glycemic index), ikiwamo mananasi na matikiti maji.

Amesema mchanganyiko huo kwa kiasi kikubwa unasababisha kupanda kwa kasi kwa sukari mwilini na kuleta unene uliopitiliza.

“Vinywaji vya sukari vimekuwa vingi na vinaleta uraibu na hivi ndio watoto wanakunywa kwa sababu ni vitamu, madhara yake ni makubwa sana baadaye. Pia tuache kabisa kuchangan-ya juisi yenye matunda mengi,” amesema Dkt. Mkeni.

Mara kadhaa, Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) - Kanda ya Afrika, Profesa Mohamed Janabi amekuwa akisisitiza watu kuzingatia lishe bora ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.

Profesa Janabi anasema kisukari na magonjwa mengine yasiyoambukiza yanatokana kwa kiasi kikubwa na mfumo wa maisha na ulaji usiofaa ikiwemo matumizi makubwa ya sukari na wanga yanayochochea ukinzani wa ‘insulin’ mwilini.

Akifafanua kuhusu uhusiano wa ulaji wa sukari na wanga, Profesa Janabi anasema; “Kula sukari na wanga kwa wingi huongeza uzalishaji wa insulin na huongeza hatari ya vifo na magonjwa mengi...”

“Na inachukua takriban miaka 10 hadi 15 kwa mtu kugundua kuwa anayo kisukari tangu ilipoanza kuathiri mwili kimya kimya.”

Ripoti ya IDF

Takwimu hizo za IDF zinaonyesha kuwa idadi inayokadiriwa ya watu wenye kisukari hapa nchini imeongezeka kutoka 134,800 mwaka 2000 hadi 472,900 mwaka 2011 kabla ya kufikia 2,928,000 mwaka 2024.

Hatari kwa matumizi

Inatoka Uk. 12

Shirikisho hilo limekadiriya kuwa idadi hiyo inatarajiwa kufikia takribani milioni 7.6 ifikapo mwaka 2050.

Uchunguzi unaonyesha ongezeko la idadi ya wagonjwa wa kisukari nchini mwaka 2000 ilikuwa takriban 134,800.

Mwaka 2011; ndani ya miaka 10 idadi hiyo iliongezeka mara tatu na kufikia watu 472,900 huku mwaka 2024 idadi ikiongezeka zaidi na kufikia watu milioni 2.9.

IDF imesema utabiri wa mwaka 2050 kwa mujibu wa utafiti wao iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa, idadi hiyo inatarajiwa kufikia watu milioni 7.8, jambo litakaloifanya Tanzania kuingia kwenye orodha ya nchi 20 zinazoongoza kwa kisukari duniani.

Nchi za ukanda wa Afrika

Takwimu zinaonyesha Tanzania imeipita Afrika Kusini na nchi zote za jirani za ukanda wa Afrika Mashariki kwa idadi ya watu wanaoishi na kisukari.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, mwaka 2000; Tanzania ilikuwa na wagonjwa wa kisukari 134,800, mwaka 2011; wakawa 472,900, huku mwaka 2024 idadi ikipanda maradufu na kufikia 2,928,000

Kwa upande wa Afrika Kusini, mwaka 2000 idadi ilikuwa 910,200 na mwaka 2011 ida-



di ikawa 1,912,400 huku mwaka 2024 ikawa 2,324,200.

Kwa Kenya mwaka 2000 idadi ya wagonjwa wa kisukari ilikuwa 202,300, huku mwaka 2011 idadi ikiwa 702,500 na mwaka 2024 idadi ikawa 1,112,800.

Nchini Uganda mwaka 2000 idadi ya wagonjwa wa kisukari ilikuwa 101,500, mwaka 2011 idadi ikawa 304,100 na mwaka 2024 idadi ikawa 553,600.

Visababishi

Kwa mujibu wa utafiti wa kitaifa hapa nchini mwaka 2023, ambao ulichapishwa katika Tanzania Journal of Health Research, ulibaini kuwa uzito au unene na shinikizo la juu la damu vilihusishwa kwa kiwango kikubwa na kisukari miongoni mwa watu wazima waliofanyiwa utafiti.

Utafiti huo ulitaja kuwa uzito uliopitiliza unasababisha kisukari kwa asilimia 50 hadi 70, ukosefu wa mazoezi na kutojishughulisha mwili asilimia 40.

Utafiti huo ulitaja pia ulaji wa vyakula mbovu asilimia 20 hadi 30, kurithi kwenye familia asilimia 10 hadi 20, umri mkubwa asilimia 10 hadi 15 huku magonjwa ya shinikizo la damu ikiwa na asilimia 5 hadi 10.

Ripoti ya WHO

Ripoti ya mwaka 2024 iliyochapishwa na jarida la The Lancet kwa ushirikiano na WHO kupitia mtandao wa NCD-RisC, idadi ya watu wazima wanaoishi na ugonjwa wa kisukari aina ya I na ya II duniani kote imezidi milioni 800.



■ Kumbukizi kifo cha Mwalimu

Nyerere angeuliza maendeleo haya yanamlinda nani?

Na Mwandishi WETU

JUMATANO, Oktoba 14, Tanzania itaadhimisha miaka 27 tangu kufariki kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hii ni kumbukizi ya kifo cha muasisi huyo wa Tanzania ambaye alifariki jijini London, Uingereza mwaka 1999 baada ya kuugua saratani ya damu. Kwa tarehe ya leo, Oktoba 11, kumbukizi hiyo ni baada ya siku tatu.

Kumkumbuka kwa fikra tunduizi kunahitaji zaidi ya picha, maua na hotuba. Kunahitaji kuuliza iwapo Tanzania inaishi misingi aliyoiamani.

Pamoja na kwamba wengi hatuwezi kujua kwa hakika angependa au kuchukua nini leo; tunaweza kupima hali yetu kwa mawazo yake kuhusu usawa, utu, uhuru na uwajibikaji.

Nyerere huenda angefurahia kuona Watanzania wakiendelea kuunganishwa na Kiswahili na utambulisho wa taifa unaoovuka makabila.

Angeona thamani katika fursa zinazowaruhusu watoto wa familia maskini kusoma, kutibiwa na kujenga maisha yenye heshima. Kwake, umoja ulihitaji kwenda pamoja na uhuru na usawa.

Lakini angeuliza swali gumu; ustawi unaotangazwa unamfikia nani? Barabara, majengo na ukuaji wa uchumi vina maana gani ikiwa mwananchi hawezi kupata haki, huduma au nafasi ya kusikilizwa?

Katika demokrasia, angeweza kuthamini uwepo wa vyama vingi na wananchi wanaojadili mustakabali wao.

Baada ya kuongoza mfumo wa chama kimoja, alisaidia kuhimiza kukubaliwa kwa ushindani wa vyama, aliweka wazi kwamba wanaoondoka CCM kuanzisha chama kingine hawapaswi kuonekana kuwa wasaliti.

Hapo ndipo urithi wake unapotuwekea mtihani. Kuwa na vyama vingi hakutoshi ikiwa mwenye mawazo tofauti anaogopa kuyasema.

Mwalimu angependa zaidi kusesitiza kuwa uchaguzi haukamilishi demokrasia ikiwa wananchi hawawezi kuwahoji viongozi, kupata taarifa na kutafuta haki bila kubaguliwa. Demokrasia hukua pale mamlaka inapokubali kuwekwa chini ya uangalizi wa wananchi.

Kwa misingi aliyotangaza, kuna sababu ya kuumini angekataa matumizi ya dola kuwanyamazisha wanaouliza maswali. Angehoji pia rushwa, upendeleo na tabia ya kugeuza madaraka kuwa njia ya kujikusanyia mali.

Hata hivyo, uchambuzi wa uaminifu haupaswi kumweka Nyerere nje ya historia. Utawala wake wa chama kimoja ulikuwa na mipaka ya ushindani wa kisiasa.

Kumheshimu hakumaanishi kuficha upungufu huo. Somo muhimu ni uwezo wa kukubali mabadiliko, kuhoji mifumo iliyopo na kutambua kwamba taifa halimilikiwi na chama kimoja.

Haki inapodumaa, umoja huwa dhaifu hata kama kimya kimetawala. Mwananchi anayenyimwa haki ya kusikilizwa habadiliki kuwa mwenye kuridhika kwa sababu tu hajapaza sauti.

Amani endelevu inahitaji mahakama zinazotenda haki, taasisi zinazowajibika na viongozi wanaoona wananchi kuwa ndiyo wenye mamlaka.

Angependa pia kuona vijana wakijiamini kuuliza, wanawake wakishiriki uamuzi na wananchi wakikataa ubaguzi, lakini sifa hizo zingepoteza maana ikiwa nafasi zinagawiwa kwa ukaribu wa wakubwa badala ya uwezo.

Mwalimu angechukizwa kuona uzalendo unaopimwa kwa utiifu kwa viongozi na kuwanyima wananchi nafasi ya kulirekebisha taifa lao. Taifa lenye kujiamini husikiliza hoja, hutenda haki na hulinda hata sauti zinazokera wenye mamlaka bila kugeuza tofauti kuwa kosa la jinai.

Kumbukizi yenye maana kwa Mwalimu Nyerere, ni kujipima kwa ujasiri na kuhoji, je, kwa sasa tunapanua uhuru au tunautengenezea viziuzi? Tunawalinda wanyonge au tunawalinda wenye nguvu?

Nyerere atakumbukwa kwa maana zaidi ikiwa utu wa mwananchi utakuwa kipimo cha maendeleo na haki haitategemea cheo, mali au msimamo wa kisiasa.



Mgombea urais adai Tucta imeporomoka

Na Mwandishi WETU

MGOMBEA nafasi ya Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), Muganga Shabani (pichani), amesema kuwa shirikisho hilo limepoteza mwelekeo na kusababisha wafanyakazi wengi kukata tamaa, hivyo linahitaji kufanyiwa maboresho makubwa.

Amesema endapo atashika nafasi hiyo, moja ya vipaumbele vyake itakuwa ni kutetea, kulinda haki za wafanyakazi bila woga wala upendeleo.

Uchaguzi Mkuu wa TUCTA unatarajiwa kufanyika Novemba 27, 2026 Jijini Dodoma. Rais wa sasa wa shirikisho hilo, Tumaini Nyamhokya, anamaliza muda wake wa vipindi viwili mfululizo.

Kwa mujibu wa Katiba ya Tucta rais wake anashika madaraka kwa vipindi viwili pekee, hivyo Nyamhokya hana sifa ya kuwania tena nafasi hiyo.

Mgombea huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Ufundi Stadi, Ushauri, Habari na Utafiti (Raawu), Tawi la Kituo cha Mafunzo na Utafiti Kilimo (MATI) - Mlingano Tanga, amesema ana vipaumbele 10 ambavyo atavitekeleza endapo atashika nafasi hiyo ya urais.

Shabani, maarufu kama 'Kilimo VPN', ametaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kutea, kulinda haki za wafanyakazi bila woga wala upendeleo.

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki, Shabani ambaye pia ni mjumbe wa Kamati Tendaji ya Raawu - Kanda ya Kaskazini na mjumbe wa mkutano mkuu wa TUCTA, amesema katika vipaumbele vyake, mali na miradi ya shirikisho vitakuwa ni kwa ajili ya kuleta manufaa na tija halisi kwa taasisi na kwa kila mfanyakazi.

"Kwa kushirikiana na wenzangu tutaimarisha umoja na mshikamano wa vyama wanachama na kuondoa migawanyiko, uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali, mapato na maamuzi yote ya Shirikisho huku tukiyapa kipa-



umbele mazungumzo yenye tija kati ya waajiri na serikali kwa maslahi ya wafanyakazi wote.

"Kipaumbele kingine ni kupigania maslahi bora, yaani mishahara stahiki, mazingira salama ya kazi na hifadhi ya jamii yenye staha," amesema.

Tucta lilianzishwa Mei 18 mwaka 2001, baada ya mabadiliko makubwa ya mfumo wa vyama vya wafanyakazi baada ya kurejea kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa na mageuzi ya sheria za ajira.

Kabla yake kulikuwa na miundo kadhaa ya vyama vya wafanyakazi, ikiwamo Juwata (1979-1991), OTTU (1991-1998) na baadaye Tanzania Federation of Free Trade Unions (TFTU).

Zamani, hususan wakati wa NUTA na Juwata, wafanyakazi walikuwa sehemu ya mfumo wa mashirika ya umma na uchumi uliokuwa ukitawaliwa zaidi na serikali, hivyo kuvifanya kuwa na nguvu na mshikamano zaidi.

Baada ya mageuzi ya uchumi, ubinafsishaji na kupungua kwa mashirika ya umma, mazingira ya wafanyakazi yalibadilika, utafiti unaonyesha kuwa ubinafsishaji na kupunguzwa kwa wafanyakazi kulipunguza kwa kiasi kikubwa msingi ambao vyama vya wafanyakazi viliutegemea.

■ Habari



Othman: Nchi za Bahari ya Hindi ziunganishe nguvu

Na Mwandishi WETU

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka nchi za ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi kuimarisha ushirikiano katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira ya bahari.

Amesema mustakabali wa uchumi wa bluu na maisha ya mamilioni ya wananchi unategemea hatua za pamoja za kuhifadhi rasilimali hizo.

Kiongozi huyo amesema ushirikiano huo ni muhimu katika kuhakikisha nchi zinazotegemea bahari kwa shughuli za uvuvi, biashara, utalii na uwekezaji zinaendelea kunufaika na rasilimali zake bila kuhatarisha mazingira na maisha ya vijazi vijavyo.

Othman ametoa mwito huo jijini Dar es Salaam wakati akifunga Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP12), uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mkutano cha Julius Nyerere (JNICC).

Akifungua mkutano huo akimwakilisha Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Othman amesema Mkataba wa Nairobi, unaolenga kulinda, kuhifadhi na kusimamia mazingira ya bahari na maeneo ya pwani, una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa wananchi wa nchi wanachama.

Amesema ushirikiano kupitia mkataba huo umesaidia kuimarisha juhudi za pamoja katika masuala ya usalama wa chakula, biashara, utalii na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

Othman amesema nchi wanachama zinapaswa kuendelea kuunganisha nguvu katika kulinda matumbawe, visiwa na mifumo mingine ya ikolojia ya bahari inayokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na shughuli za binadamu.

Mkataba wa Nairobi unazihusisha nchi za Kenya, Tanzania, Msumbiji, Afrika Kusini, Comoro, Mauritius, Shelisheli, Somalia, Madagascar na Ufaransa.

Utegemezi uchumi wa buluu

Othman amesema wakati nchi za ukanda huo zikiendelea kuwekeza katika uchumi wa buluu, ni lazima suala la uhifadhi wa mazingira lipewe kipaumbele ili kuhakikisha shughuli za kiuchumi zinazotegemea bahari zinakuwa endelevu.

Ameeleza kuwa uwekezaji katika sekta za bahari unapaswa kwenda sambamba na hatua za kulinda rasilimali zake, huku wanawake na vijana wakipewa nafasi kubwa zaidi ya kushiriki na kunufaika na fursa zinazopatikana.

Amesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, jumuiya za kijamii na wadau wa maendeleo katika kukabiliana na mazingira ya kimazingira.

“Changamoto za mazingira haziwezi kutatuliwa na nchi moja pekee, hivyo kuna umuhimu wa kuwa na mikakati ya pamoja inayotekelezeka katika ngazi za kitaifa na kikanda,” ameingiza.

Zanzibar yasisitiza uhifadhi

Akizungumzia Zanzibar, Othman amesema bahari siyo rasilimali ya kiuchumi pekee, bali pia ni sehemu muhimu ya urithi, utamaduni na maisha ya wananchi wa visiwa hivyo.

Amesema Serikali ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali na jumuiya za wananchi katika kutekeleza programu za uhifadhi wa mazingira ya bahari na maeneo ya pwani.

Ametaja juhudi zinazofanywa na vikundi vya kijamii, wakiwamo wanawake wanaojishughulisha na uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya Pemba, kuwa mfano wa umuhimu wa wananchi kushiriki moja kwa moja katika kulinda rasilimali za asili.



Uchumi & Biashara

Benki ya Dunia yaibua mambo 10 kukua uchumi wa Tanzania

Uchumi unakua kwa kasi, lakini uwekezaji mdogo wa kampuni, ajira zisizo rasmi na tija ndogo vinatajwa kuwa vikwazo vikubwa kwa maendeleo ya biashara na ongezeko la kipato cha Watanzania.

Na Mwandishi WETU

WAKATI uchumi wa Tanzania ukitarajiwa kukua kwa asilimia 6.1 mwaka huu, Benki ya Dunia imeibua changamoto 10 zinazokwamisha ukuaji wa biashara, uwekezaji na ajira zenye tija.

Sambamba na hilo, benki hiyo imeonya kuwa kasi ya ukuaji wa uchumi pekee haitoshi kuboresha maisha ya wananchi.

Katika ripoti yake mpya ya Tanzania Economic Update: Making Jobs Work, Benki hiyo inaonyesha kuwa Tanzania imepiga hatua kudumisha utulivu wa uchumi, lakini bado inakabiliwa na udhaifu wa kimundo unaozuia sekta binafsi kuzalisha ajira bora na kuongeza kipato cha wananchi.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, uchumi ulikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na unatarajiwa kufikia asilimia 6.1 mwaka 2026, kabla ya kuimarika hadi wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi cha muda wa kati.

Hata hivyo, nyuma ya takwimu hizo kuna hali inayotia wasiwasi; asilimia 95 ya ajira nchini ni zisizo rasmi, kampuni nyingi haziongezi uwekezaji na mamilioni ya Watanzania wanaendelea kufanya kazi zenye kipato kidogo.

Kwa maneno mengine Benki ya Dunia inasema kuwa Tanzania ina fursa kubwa za ukuaji, lakini kuzitumia fursa hizo kunahitaji mageuzi katika mazingira ya biashara, upatikanaji wa mitaji, ardhi, teknolojia na ujuzi wa wafanyakazi.

Serikali yabeba mzigo wa ukuaji

Changamoto ya kwanza inayobainishwa na ripoti hiyo ni utegemezi mkubwa wa matumizi ya serikali katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Benki ya Dunia inaeleza kuwa zaidi ya theluthi mbili ya ukuaji halisi wa uchumi mwaka 2025 ulitokana na matumizi ya Serikali, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 45 katika kipindi cha mwaka 2021 hadi



2024. Hii ina maana kuwa ingawa sekta binafsi inaendelea kuchangia uchumi, kasi yake ya uwekezaji na matumizi haijawa kubwa kutosha kuwa injini kuu ya ukuaji.

Sekta za huduma, hususan fedha, usafirishaji na biashara, zilichangia karibu nusu ya ukuaji wa uchumi kwa upande wa shughuli za uzalishaji.

Kwa mtazamo wa kibiashara, hali hiyo inaibua swali kuhusu uwezo wa sekta binafsi kuendeleza kasi ya ukuaji iwapo matumizi ya serikali yatapungua.

Hali hiyo pia inaleta wasiwasi kuhusu utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo sekta binafsi inapaswa kuchangia utekelezaji wake kwa asilimia 70.

Kwa mujibu wa watalaamu wa uchumi, miradi mikubwa ya umma inaweza kufungua masoko na kuboresha miundombinu, lakini manufaa yake ya muda mrefu yanategemea uwezo wa kampuni binafsi kutumia fursa hizo kuongeza uzalishaji na uwekezaji.

Ajira zipo, lakini kipato kidogo

Changamoto ya pili iliyoanishwa katika ripoti hiyo ni ubora wa ajira nchini.

Ripoti inaonyesha kuwa asilimia 68.7 ya Watanzania wenye umri wa kufanya kazi walikuwa wameajiriwa au kujishughulisha na shughuli za kiuchumi mwaka 2024.

Inaendelea Uk. 18

■ Biashara

Benki ya Dunia...

Inatoka Uk. 17

Kwamba kipato cha kati kwa saa kwa watu walio-ajiriwa kilikuwa Shilingi 1,005 pekee.

Hii inaonyesha kuwa tatizo kubwa siyo ukosefu wa shughuli za kufanya, bali ni uwezo wa shughuli hizo kuzalisha kipato kinachokidhi mahitaji ya mai-sha.

Kwa mujibu wa benki hiyo, wafanyakazi wanaopokea mishahara kutoka kwa waajiri wanawakilisha asilimia nane pekee ya nguvu kazi, huku wengi waki-ajiri au kufanya kazi katika shughuli za familia.

Hali hii ina athari za moja kwa moja kwa biashara kwa sababu kipato kidogo cha wananchi kinapunguza uwezo wao wa kununua bidhaa na huduma, hivyo kudumaza shughuli za kibiashara.

Kadiri kipato cha kaya kinavyokuwa kidogo, ndivyo soko la ndani linavyoshindwa kukua kwa kasi inayoweza kuvutia uwekezaji mkubwa wa viwanda na huduma.

Asilimia 95 ajira zisizo rasmi

Changamoto ya tatu ni ukubwa wa sekta isiyo rasmi.

Ripoti inaonyesha kuwa ajira zisizo rasmi ziliongezeka kutoka takribani asilimia 93 mwaka 2020 hadi asilimia 95 mwaka 2024.

Hii ina maana kuwa karibu wafanyakazi 95 kati ya 100 wanafanya kazi katika mazingira yasiyo rasmi.

Kwa uchumi, hali hiyo inaathiri ukusanyaji wa kodi, upatikanaji wa hifadhi ya jamii, uwezo wa biashara kupata mikopo na uwekezaji wa muda mrefu.

Lakini benki hiyo inaonyesha kuwa kurasimisha biashara pekee hakutoshi na kinachohitajika ni mazingira yanayowezesha biashara ndogo kukua, kuongeza uzalishaji, kuajiri wafanyakazi na kumudu gharama za kufanya shughuli rasmi.

Kwa hiyo, sera za kurasimisha biashara zinahitaji kwenda sambamba na upatikanaji wa mitaji, masoko na teknolojia.

Kilimo kinabeba uchumi wa ajira

Changamoto ya nne ni utegemezi mkubwa wa kilimo na benki hiyo inaeleza kuwa asilimia 54 ya wafanyakazi nchini wanajishughulisha na kilimo, wakati

huduma zinaajiri takribani theluthi moja na viwanda karibu asilimia 10.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya shughuli za kilimo bado ina tija ndogo.

Hali hii ina maana kuwa kuongeza kipato cha Watanzania kunahitaji kuwekeza zaidi katika kilimo cha kisasa, umwagiliaji, mbegu bora, mbolea, mashine na viwanda vya kuchakata mazao.

Kwa wawekezaji, kilimo kinawakilisha mojawapo ya fursa kubwa za biashara, hususan katika kuongeza thamani ya mazao, uhifadhi, usafirishaji na uzalishaji wa chakula.

Ajira bora ni chache mno

Changamoto ya tano ni uhaba wa ajira zenye mishahara mizuri, mikataba rasmi na hifadhi ya jamii.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa kati ya ajira takribani milioni 26 nchini, ni ajira 550,000 pekee zinazokidhi vigezo vya ubora wa juu.

Kati ya hizo, ajira 120,000 tu zinapatikana katika sekta binafsi.

Hii ina maana kuwa ni takribani ajira mbili kati ya 100 zinazokidhi vigezo hivyo.

Ripoti inaonyesha pia kuwa karibu nusu ya ajira bora za sekta binafsi zinapatikana Dar es Salaam.

Hali hiyo inaonyesha umuhimu wa kupanua uwekezaji wa kampuni zenye uwezo wa kutoa ajira bora katika mikoa mingine, badala ya fursa hizo kujikita katika jiji moja.

'Vijana ni bomu'

Changamoto ya sita ni kasi ya ongezeko la nguvu kazi, ambapo benki hiyo inakadiria kuwa Watanzania takribani milioni mbili wanafikia umri wa kufanya kazi kila mwaka, wakati takribani 400,000 wanaondoka katika kundi hilo kutokana na kustaafu au vifo.

Hivyo, kundi la watu wenye umri wa kufanya kazi linaongezeka kwa takribani milioni 1.6 kwa mwaka.

Kwa upande mmoja, hali hiyo inatoa fursa ya kuwa na nguvu kazi kubwa na soko pana la bidhaa na huduma.

Lakini bila uwekezaji wa kutosha katika biashara na viwanda, vijana wengi wanaweza kuendelea kuingia katika shughuli zisizo rasmi zenye kipato kidogo.

Inaendelea Uk. 19

Biashara ■

Benki ya Dunia...

Inatoka Uk. 18**Kampuni mpya ni chache**

Changamoto ya saba ni kasi ndogo ya kuanzishwa kwa kampuni rasmi ambapo ripoti inaonyesha kuwa mwaka 2023, asilimia 12 pekee ya kampuni rasmi Tanzania zilikuwa zimeanzishwa baada ya mwaka 2018.

Kwa kulinganisha, kiwango hicho kilikuwa asilimia 38 nchini Rwanda na asilimia 26 chini ya kiwango cha Ghana. Benki ya Dunia inaeleza kuwa Tanzania imefanya maboresho katika mifumo ya usajili wa biashara, lakini bado kuna changamoto za gharama, muda na taratibu za kuanzisha kampuni.

Kwa wawekezaji, hali hiyo inaashiria umuhimu wa kurahisisha zaidi mazingira ya kuanzisha na kukuza biashara mpya.

Uwekezaji kampuni waporomoka

Changamoto ya nane, na ambayo inaleta wasiwasi zaidi, ni kupungua kwa uwekezaji unaofanywa na kampuni. Benki ya Dunia inaeleza kuwa wastani wa uwekezaji wa kampuni nchini umefikia asilimia 11 tu ya kiwango kilichokuwapo miaka 10 iliyopita.

Kwa maana nyingine, kampuni kwa wastani zinaweza kiasi kidogo sana katika mashine, teknolojia, miundombinu na upanuzi wa shughuli zake ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Hali hii inaweza kuathiri uwezo wa Tanzania kuongeza uzalishaji na kushindana katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Bila uwekezaji katika teknolojia na mbinu mpya za uzalishaji, kampuni zinaweza kuendelea kufanya biashara, lakini zikashindwa kuongeza tija na mishahara ya wafanyakazi.

Mitaji na ardhi bado vikwazo

Changamoto ya tisa ni upatikanaji wa fedha na ardhi kwa shughuli za biashara.

Ripoti inaonyesha kuwa kampuni moja kati ya tatu inakabiliwa na vikwazo vya kupata mikopo, huku asilimia 58 ya kampuni kubwa zikitaja upatikanaji wa ardhi kuwa kikwazo kikubwa.

Hali hiyo inajitokeza licha ya mikopo kwa sekta binafsi kuongezeka kwa asilimia 28.1 katika mwaka ulioishia Juni 2026. Kwa hiyo, changamoto si kiasi

cha fedha kinachokopeshwa pekee, bali pia aina ya mikopo, masharti na uwezo wa kampuni kupata mitaji ya muda mrefu.

Kwa biashara zinazotaka kuwekeza katika viwanda, mashine na upanuzi wa uzalishaji, upatikanaji wa mitaji yenye masharti yanayofaa ni jambo muhimu.

Elimu, ujuzi havikidhi mahitaji

Changamoto ya 10 ni pengo kati ya elimu na mahitaji ya soko la ajira.

Benki hiyo inakadiria kuwa wastani wa miaka ya elimu iliyorekebishwa kwa kuzingatia kiwango cha kujifunza kwa watu wazima nchini ni takribani miaka 4.5. Aidha, zaidi ya nusu ya wafanyakazi wanakabiliwa kwa pamoja na kiwango kidogo cha utayari wa kufanya kazi zenye tija na fursa finyu za soko.

Ripoti inaonyesha kuwa wafanyakazi wenye elimu ya sekondari ya chini hupata mishahara iliyo juu kwa asilimia 22 hadi 30 katika ajira rasmi za sekta binafsi ikilinganishwa na wenye elimu ya msingi pekee.

Hii inaonyesha kuwa elimu bora, mafunzo ya ufundi na ujuzi wa kiteknolojia ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na ushindani wa biashara.

Nini kifanyike?

Kwa ujumla, uchambuzi wa Benki ya Dunia unaonyesha kuwa Tanzania haikabiliwi na tatizo la ukuaji mdogo wa uchumi, bali changamoto ya kuhakikisha ukuaji huo unazalisha biashara zenye tija, ajira bora na kipato kikubwa zaidi.

Kwa serikali, kipaumbele kinapaswa kuwa kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kupunguza vikwazo vya biashara na kuwezesha kampuni kukua.

Kwa sekta binafsi, changamoto ni kuongeza uwekezaji katika teknolojia, ubunifu, uzalishaji na mafunzo ya wafanyakazi.

Kwa taasisi za fedha, kuna umuhimu wa kupanua upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu kwa biashara zinazotaka kuongeza uzalishaji.

Na kwa mfumo wa elimu, jukumu ni kuhakikisha vijana wanaomaliza masomo wanakuwa na ujuzi unaohitajika katika uchumi wa kisasa.

Hatimaye, mafanikio ya Tanzania kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hayatapimwa kwa kasi ya ukuaji wa pato la taifa pekee, bali kwa uwezo wa uchumi huo kuongeza kipato cha wananchi na kuwa na kampuni zinazoweza kushindana katika masoko ya ndani na kimataifa.

■ Uchambuzi

Freeman Mbowe ni konokono na mwanzi wa kisiasa



Freeman Mbowe

Na Ansbert NGURUMO

MASHAMBULIZI dhidi ya demokrasia ni hatari kwa jamii yoyote. Lakini hatari nyingine ni pale wanaopinga udikteta wanapoanza kutumia mbinu za kidikteta dhidi ya watu wasiokubaliana nao.

Wengi tumekuwa tukikemea udikteta na kuendelea kupinga vitendo vya kiimla vya watawala, hatuna sababu ya kufumbia macho tabia hizo zinapojitokeza miongoni mwa wapigania demokrasia.

Tuliporejesha mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, hatukukusudia kuongeza vyama pekee, bali kupanua uhuru wa mawazo, ushindani wa hoja na uvumilivu wa kisiasa. Ni hatari kurejesha fikra za chama kimoja huku tukijigamba kupigania mabadiliko.

Kinachonisumbua sasa ni utamaduni wa 'group-think,' ambapo watu wanashinikizwa kufikiri sawa na kundi fulani. Mtu anayetoa hoja tofauti anashambuli-

wa ili kumnyamazisha yeye na wengine wenye maoni kama yake. Huu ni udikteta wa kimawazo unaoweza kuzaa utamaduni wa kisiasa usiovumilia tofauti.

Nimeushuhudia katika mashambulizi dhidi ya andiko langu kuhusu urathi wa Freeman Mbowe. Baadhi ya wakosoaji wamejibu hoja; wengine wamenishambulia binafsi, kana kwamba kutambua mchango wa Mbowe ni kosa. Hawataninyamazisha. Wamenichochea kusema zaidi.

Mbowe amebadilika au siasa zimembadilikia?

Mbowe ninayemfahamu kwa miaka mingi ni mfanyabiashara kabla hajawa mwanasiasa. Alikulia katika familia ya wafanyabiashara, akafanya kazi Benki Kuu ya Tanzania na baadaye kujihusisha na biashara za familia.

Chadema ilipoanzishwa mwaka 1992, yeye alikuwa miongoni mwa waasisi; alibeba fikra za ujasiriamali, uchumi wa soko na uhuru wa mtu binafsi, ambazo pia zilikuwa sehemu ya falsafa ya waasisi wenzake ws chama hicho, akiwamo Edwin Mtei. Hakuwahi kuamini kwamba mwanasiasa lazima awe maskini ili awe mzalendo.

Mbowe ninayemfahamu ni mwanamikakati na mjenzi wa taasisi. Alielewa mapema kwamba chama hakiwezi kukua kwa hotuba pekee; kinahitaji fedha, watu, ofisi, usafiri, mawasiliano na mipango.

Mwaka 2000, Chadema ilikuwa na wabunge watano, lakini alishiriki kuandaa na kugharamia kampeni zilizowapeleka wabunge wenzake mikoani kupinga kodi ya maendeleo, iliyofutwa mwaka 2003. Alisaidia kuonyesha kwamba wabunge wachache wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa nje ya bunge iwapo watapangwa vizuri.

Mbowe ninayemfahamu ni mbunifu wa mikakati ya kisiasa. Kampeni yake ya urais ya mwaka 2005, iliyotumia helikopta, haikuwa usafiri pekee; bali ilikuwa mkakati wa kuitangaza Chadema kitaifa. Alipata asilimia 5.88 ya kura za urais, lakini chama kikapata wabunge 11 na madiwani 103.

Mwaka 2010, mgombea wa Chadema, Dkt. Willibrod Slaa, alipata asilimia 27.1 ya kura; mwaka 2015, Edward Lowassa alipata karibu asilimia 40 kupitia ushirikiano wa 'Ukawa.' Mafanikio hayo yalikuwa ya wengi, lakini Mbowe alikuwa mmoja wa wabunifu na wawezeshaji wake wakuu.

Inaendelea Uk. 21

Uchambuzi ■

Freeman Mbowe...

Inatoka Uk. 20

Mbowe ninayemfahamu ni mlezi wa vipaji. Alita-futa watu wenye uwezo popote walipokuwa, akawapa nafasi, akawaamini na kuwajenga. Wengine walikuja kuwa viongozi wenye nguvu na ushawishi mkubwa, hata kufikia hatua ya kushindana naye. Akikaa nyuma yao, akawatanguliza, wakasaidiana kujenga taasisi iliyowawezesha wengi wao kung'ara.

Mbowe ninayemfahamu ni mwanadiplomasia. Ana marafiki katika vyama mbalimbali, hata CCM. Ni mjenzi wa madaraja. Tangu enzi za Rais Benjamin Mkapa, Mbowe amekuwa akitumia mazungumzo, shinikizo na mikakati ya kisiasa kujenga Chadema katika mazingira ambayo vyama vingine vingi vya upinzani vilishindwa kupata nguvu zinazolingana nayo.

Aliendeleza mtazamo huo wakati wa Rais Jakaya Kikwete, Rais Magufuli na Rais Samia Suluhu Hassan. Kwake, kuzungumza na mpinzani siyo kujisali-misha; bali ni kutafuta fursa ya nafuu fulani au suluhu.

Mbowe ninayemfahamu ni mtu mwenye ustahimilivu mkubwa. Kati ya mwaka 2016 na 2021, utawala wa Rais Magufuli ulibana shughuli za kisiasa za Chadema, huku biashara zake zikikabiliwa na hatua kali za dola, zikiwamo taarifa za kufungwa kwa shughuli na kuzuiwa kwa akaunti zake.

Alikabiliwa na kesi, kukamatwa na hatimaye kifungo cha zaidi ya miezi saba mwaka 2021-2022, lakini hakufanya mateso yake binafsi kuwa kampeni ya kutafuta huruma. Mara nyingi alizungumza zaidi kuhusu madhila ya chama na wananchi kuliko yaliyompata yeye mwenyewe.

Mbowe ninayemfahamu siyo mwepesi wa kujibu mapigo. Huzungumza kwa nadra, hupendelea kupanga mikakati kuliko mabishano hadharani, na siyo rahisi kumwona akijitetea dhidi ya kila tuhuma.

Nimezoea kumsikia akikosoa wengine, na inapobidi kuwapa sifa zao, lakini sikumbuki kumsikia akimtukana mtu jukwaani. Hulka yake ni tofauti.

Na hapa ndipo ninaamini baadhi ya walioanzisha au kuendeleza propaganda za sasa kumharibia sifa walipotambua nafasi ya kumshambulia.

Walijua kwamba siyo mwepesi wa kujibu, na kwamba ukimya wake ungeweza kuacha tuhuma



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Freeman Mbowe Ikulu jijini Dar es Salaam. Machi 5, 2022

zirudiwe bila kupingwa hadi zikaanza kuaminika. Ustahimilivu uliomsaidia kuvuka dhoruba nyingi za kisiasa ukawa pia udhaifu unaoweza kutumiwa dhidi yake.

Mbowe ninayemjua ni mwanasiasa mwangalifu anayejua wakati wa kuuma na wakati wa kupuliza; na vipaji hivi ndivyo alitumia kujenga Chadema hii iliyojitofautisha na vyama vingine.

Kwa hiyo, ninapomwona Mbowe akizungumza na Rais Samia, akihudhuria baadhi ya shughuli za serikali, akipongeza jambo zuri au akinyamaza anaposhambuliwa, sioni mtu mpya. Namwona Mbowe yuleyule mpatanishi.

Namfahamu Mbowe kama konokono na mwanzi wa kisiasa. Anafanya siasa kwa subira, tahadhari na ustahimilivu, bila papara, huku akiacha alama ya mchango wake kila anapopita.

Kama mwanzi, huinama mbele ya dhoruba kali za kisiasa bila kuvunjika, na dhoruba zinapopita husimama tena wima, tayari kuendelea na safari yake.

Kuyasema haya siyo kumpa sifa bandia, bali kuweka hadharani hulka zake ambazo zimekuwa chachu ya mafanikio ya kisiasa ya chama alichojenga.

Ni historia isiyofutika aliyoiandika kwa vitendo. Naiandika nikichochea na mijadala hasi anayofanyiwa mfululizo kwa miaka ipatayo miwili sasa, ili wanaojaribu kufuta ukweli huu wapate ubavu wa ku-shikilia wanaposhikana mieleka na historia.

Inaendelea Uk. 22

■ Uchambuzi

Freeman Mbowe...

Inatoka Uk. 21

Mbowe naye ana mizigo yake

Kumwelewa Mbowe hakumaanishi kumtakasa. Katika miaka 21 ya uenyekiti wake, pamoja na uwezo mkubwa wa uongozi na busara iliyosaidia Chadema kuvuka dhoruba nyingi za dola, wapo watu walioumizwa naye kisiasa.

Baadhi yao walikwazwa na uamuzi wake mwenyewe; wengine waliuamizwa na vitendo vya watu wake wa karibu, wafuasi wake au wale walioitwa “vijana wake.” Sasa wamepata upenyo wa kulipiza kisasi.

Siyo kila aliyekuwa na malalamiko dhidi yake alikuwa na nia mbaya. Baadhi yao wanaweza kuwa na sababu za msingi za kumlaumu.

Ninaamini pia kwamba miongoni mwa wanaomshambulia sasa wapo waliobeba machungu ya muda mrefu, ambao wameona mabadiliko ya uongozi kuwa fursa ya kumshughulikia kisiasa. Hiyo ni mizigo yake. Aibebe.

Kiongozi hawezi kudai sifa zote za mafanikio ya taasisi yake, halafu akajitenga na makosa yaliyofanyika chini ya uongozi wake. Mbowe anapaswa kuwajibika kwa uamuzi wake, makosa yake binafsi na

vitendo vya watu aliowapa mamlaka au ushawishi, pale anapohusika.

Huwezi kuongoza chama kwa miaka 21 bila hatari ya kufanya makosa yatayokuandama. Huenda baadhi ya migogoro hii inatokana na ukweli huo.

Wapo pia waliomuunga mkono wakati wa kampeni, aliposhindwa wakaona njia ya kujikubalisha kwa uongozi mpya ni kufuata mbinu yao mpya ya kumtutkana na kumdhalilisha. Ni mbinu yao.

Lakini kuwajibika siyo sawa na kudhalilishwa. Makosa ya Mbowe hayahalalishi matusi, propaganda au jitihada za kufuta historia. Aliyekosewa ana haki ya kudai haki, lakini hiyo siyo leseni ya kutenda dhuluma nyingine.

Kinachofanyika sasa miongoni mwa baadhi wa makada, wafuasi na wanaharakati wa Chadema hakina tofauti na tulichoshuhudia wakati wa utawala wa Magufuli, pale vijana waliopewa vyeo walipoamua kutumia vyombo vya habari na majukwaa ya siasa kutukana viongozi wastaafu waliokuwa na maoni tofauti na ya rais - ili kuwanyamazisha. Tuliwakemea. Iweje tunawashangilia hawa wa sasa?

Mazungumzo na serikali siyo usaliti

Baada ya kuachiwa gerezani Machi 4, 2022, Mbowe jioni alienda Ikulu kukutana na Rais Samia. Tukio hilo lilishangaza kila mtu. Picha yao ilisambaa usiku huohuo na kuzua tafsiri mbalimbali, lakini haikueleza juhudi za viongozi kadhaa wa dini waliokuwa wamehusika kusababisha tukio hilo.

Nafahamu kwa karibu kutoka kwa baadhi yao juu ya mchakato huo, kwamba awali, baada ya kukubaliana nao, Mbowe alitaka kukutana kwanza na viongozi wenzake wa chama kabla ya kwenda Ikulu, lakini baadaye alikubali ushauri wa wapatanishi.

Mazungumzo yaliyofuata yalichangia kubadili upepo wa kisiasa na kukata minyororo iliyofungwa na awamu ya Magufuli. Mikutano ya hadhara ikarejeshwa Januari 2023, baadhi ya viongozi waliokuwa uhamishoni wakarejea, mazungumzo ya mageuzi ya kisiasa na uchaguzi yakaanza, wanachadema wapatao 400 nchi nzima waliokuwa wamefungwa au wanakabiliwa na kesi mbalimbali wakaachiwa, upinzani ukaanza tena kupumua.



Rais John Magufuli akizungumza na Freeman Mbowe wakati wa msiba wa Meja Jenerali Mstaafu Albert Mbowe alipofika nyumbani kwa marehemu Salasala jijini Dar es Salaam. Julai 30, 2019

Inaendelea Uk. 23

Uchambuzi ■

Freeman Mbowe...

Inatoka Uk. 22

Hiyo ilikuwa sehemu ya mafanikio, ndicho pia kiligeuzwa kitanzi cha Mbowe. Sababu zake ni uchambuzi mwingine kabisa. Itoshe tu kusema kuwa mazungumzo haya hayakutimiza kila matarajio.

Katiba mpya haikupatikana, mageuzi muhimu yalibaki bila kukamilika na hatimaye kuaminiana kati ya pande hizo kukatoweka.

Ni halali kuhoji kama Mbowe alimwamini Rais Samia kupita kiasi, au kama mazungumzo hayo yalikuwa na uwazi wa kutosha, lakini kushindwa kwa mkakati siyo uthibitisho wa usaliti.

Lakini wafuatiliaji wa masuala haya wanatambua kuwa Rais Samia hakumbadilisha Mbowe kuwa mwanadiplomasia. Alimkuta akiwa hivyo kwa miaka mingi.

Kilichomkuta Mbowe ni kile walichosema wahenga wa Uingereza: “give a dog a bad name and kill him.” Ukitaka kumuua mbwa, mtangaze kote kuwa ni mwizi.

Chadema isiyoweza kukimbia historia yake

Tukubaliane kuwa kilichobadilika zaidi ni mazingira ya kisiasa na mbinu za baadhi ya viongozi na wafuasi wa Chadema. Kizazi kilnachopitia ukandamizaji, uchaguzi usio halali, vitisho, mateso na mauaji ya raia, kinaamini kuwa mapambano na minyukano isiyo na simile ndicho kipimo kikuu cha uaminifu.

Kwao, mazungumzo ni udhaifu. Wengine wanasema ni usaliti. Hisia hizo zinaeleweka. Lakini hazibadilishi historia.

Kihistoria, Chadema ilijengwa kwa kuchanganya mikakati: ushawishi, maandamano, kampeni, operesheni, mashinikizo, mazungumzo, ushirikiano wa kisiasa na matumizi ya rasilimali.

Haiwezekani sasa kugeuza baadhi ya mbinu hizo kuwa ushahidi wa usaliti kwa sababu tu uongozi mpya unaamini katika minyukano pekee.

Januari 2025, Mbowe alishindwa uenyekiti kwa kura 482 dhidi ya 513 za Tundu Lissu. Tofauti ya kura 31 ilionyesha ushindani mkali, siyo kukataliwa na chama kizima.

Mbowe alikubali matokeo na kuondoka. Akaa-ga na kusema sasa amepata fursa ya kwenda kutengeneza “mafekeche.” Ndiko aliko, na ndiko huko

anakojomewa Akionekana anapigwa. Asipoonekana anapigwa. Akinyamaza anapigwa. Akisema anapigwa. Akisemwa vizuri wanaosema wanapigwa.

Ndicho kilichomkuta alipomtembelea Tundu Lissu gerezeni. mashabiki wa Lissu wakadai amepeleka summer. Hakwenda mahakamani, wakasema amem-susia kesi.

Alipohudhuria uzinduzi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere Agosti 2026 na kupongeza kukamilika kwake, akashambuliwa mitandaoni. Septemba 10, alipomtembelea Rais Samia Kizimkazi kumpa pole kwa msiba wa mumewe, akatuhumiwa tena.

Hapa ndipo ‘confirmation bias’ inapojitokeza; mtu akishahukumiwa kuwa msaliti, kila tendo lake hutafsiriwa kuthibitisha hukumu hiyo. Akizungumza, anatumia, akikaa kimya, anatumia. Aki-kutana na watawala, anatumia. Hata akifanya jambo la kibinadamu, nia yake inahojiwa.

Nionavyo mimi, Chadema ina haki ya kubadili mbinu zake. Inaweza kuamua kwamba diplomasia iliyotumika zamani haifai katika mazingira ya sasa. Inaweza kuchagua makabiliano makali zaidi.

Lakini haina sababu ya kumlazimisha Mbowe abadili hulka yake ili aonekane mwaminifu kwa mwelekeo mpya.

Na haiwezi kuandika historia yake kwa uaminifu kwa kuzigeuza mbinu zilizosaidia kuijenga kuwa makosa ya kisiasa. Huo ni uandishi mbovu wa historia.

Umaarufu siyo urathi

Hata kama Mbowe amefanya makosa, au taswira yake mbele ya jamii imebadilika, urathi wake wa kisiasa unabaki imara. Umaarufu wa mtu na urathi wake ni mambo mawili tofauti.

Umaarufu wa mtu unaweza kupanda au kushuka kutokana na makosa, propaganda na mabadiliko ya mitazamo ya jamii. Lakini urathi wake hupimwa kwa kile ambacho alijenga, alichobadilisha na alichocha katika historia.

Wakati najadili hoja hii nimemkumbuka mcheza soka Diego Maradona. Aliiongoza Argentina kutwaa Kombe la Dunia mwaka 1986, na kuibadilisha Napoli ya Italia kutoka klabu ndogo mno ya soka hadi kutwaa ubingwa wa Serie A mwaka 1987 na 1990, pamoja na Kombe la UEFA mwaka 1989. Maradona akawa alama ya fahari ya Napoli na shujaa wa taifa lake.

Inaendelea Uk. 28

■ **Kilinge cha Mawasiliano**

Na Loth MAKUZA

Majoho ya mahafali siyo matokeo

KILA Desemba vyuo vikuu vingi hufanya jambo moja kwa ustadi mkubwa; vinajipanga vyema kuhakikisha sherehe kubwa kwa wanafunzi kuhitimu masomo yao.

Katika pilikapilika hizo, majoho yanaandaliwa na kuvaliwa, ngoma zinapigwa na picha zinafika WhatsApp kabla jina la mwisho la mhitimu hali-jasomwa.

Ni siku nzuri, lakini kutoka nje ya geti uulize swali dogo kwamba chuo hiki kimetatusa tatizo gani la nchi mwaka huu? Ukimya unaweza kuwa mzito.

Inawezekana mengi yametatuliwa, lakini haku-na aliyetuambia.

Hapa ndipo mawasiliano ya kimkakati katika elimu ya juu yanapoacha kuwa pambo na kuwa su-ala la umuhimu wa kuwepo.

Ushawishi wa chuo kikuu haupaswi kupimwa kwa idadi ya wanafunzi kinaowahitimu pekee, bali kwa matatizo kinayosaidia jamii kuyatatua.

Hotuba ya ufunguzi ya Prof. Eliamani Sedoyeka, Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA), katika Kongamano na Maonyesho ya Nne ya Kimataifa ya Utalii Arusha (AITC 2026), ilinirudishia wazo hili.

Alisema waziwazi kwamba taasisi za elimu ya juu lazima ziwe wachangiaji hai wa maendeleo ya taifa, na wajibu wao unavuka ufundishaji darasani.

Mkuu huyo wa chuo aliielezea AITC kama jukwaa linalowakutanisha wanaozalisha maarifa na wanaoyatumia, ambapo watafiti wanaisikiliza sekta na watunga sera wananufaika na ushahidi.

Watafiti wanachapisha katika majarida ambayo katibu mkuu hayafungui kamwe, huku mwendeshaaji wa utalii hasikii kwamba mhadhiri aliye jirani amelitafiti tatizo lake. Maarifa yamelala kwenye PDF, matokeo yanasubiri nje.

Basi niulize; vyuo vyetu vinawasilisha maarifa, au vinawasilisha matokeo? Utafiti ni maarifa.

Taasisi nyingi huyachukulia mawasiliano kama mpigapicha anayefika baada ya kazi kwisha; piga picha, toa taarifa kwa vyombo vya habari, basi.

Mawasiliano ya kimkakati katika elimu ya juu yanapaswa kuja mwanzo, siyo mwisho. Yanauli-za wadau wetu ni akina nani, wanatarajia nini, na kama tupo ndani ya chumba ambamo mijadala ya kitaifa inafanyika. Ni kazi ya kiuongozi, si kujitan-gaza tu.

Utalii, kwa mujibu wa mkuu huyo wa chuo, unachangia zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa na takribani robo ya mapato ya fedha za kigeni.

Mwaka 2025 nchi ilipokea watalii wa kimataifa zaidi ya milioni 2.29 na mapato ya takribani dola za Marekani bilioni 4.41.

Pia alisisitiza kwamba utalii uwezeshwe na teknolojia lakini uongozwe na watu.

Sasa fikiria nafasi inayofunguka hapa; chuo kikuu kimesimama pale ambapo utalii unakutana na teknolojia, utafiti, ujuzi, uwekezaji, serikali na maendeleo ya jamii.

Hii ni kazi yangu ya nyumbani kwa kila chuo kikuu Tanzania na Afrika nzima. Kabla ya mahafali yajayo, jibuni maswali matano.

Tunatatua tatizo gani? Tunazalisha maarifa gani? Nani anayatumia? Nini kimebadilika kwa sababu ya kazi yetu?

Tunaitengenezea jamii thamani gani? Kama hamuwezi kuyajibu, tatizo si ofisi yenu ya mawasiliano. Kama mnaweza kuyajibu lakini hakuna anayejua, basi tatizo ni la ofisi hiyo.

Jamii ina shughuli nyingi. Hakuna atakayekuja kugundua thamani yenu.

Mawasiliano ya kimkakati katika elimu ya juu ndiyo njia ya chuo kutoka nje ya geti lake, joho na vyote, na kwenda pale ambapo maamuzi ya maendeleo ya taifa na fursa za sekta yanafanyika.

Mahafali ni sherehe na matokeo ni mazungumzo. Vyuo vyetu lazima vijifunze kushika vyote viwili.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@loth-makuza.co.tz



Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Ni hatari kwa mgonjwa kufanya mazoezi 'gym'

KATIKA juhudi za kurejesha afya na uwezo wa mwili baada ya kupata kiharusi (stroke), familia na wagonjwa wengi wamekuwa wakikimbilia kumbi za mazoezi (gym) kama njia ya mkato ya kusaidia mgonjwa apone.

Hata hivyo, wataalamu wa afya wanatoa tahadhari kubwa; ingawa mazoezi yaliyopangiliwa kitaalamu ni nguzo kuu ya uponyaji, kuingia gym bila usimamizi wa kitaalamu kunaweza kubadilisha matumaini ya kupona kuwa janga lingine la kiafya.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa mwili wa mtu aliyepona kiharusi unahitaji umakini wa pekee.

Kufanya mazoezi ya nguvu kubwa au kutumia vifaa visivyo sahihi kunamweka mgonjwa katika hatari zifuatazo.

Kwanza ni kupanda kwa kasi kwa shinikizo la damu na mapigo ya moyo. Mazoezi ya kuinua vyuma vizito au kufanya mazoezi yanayokaza misuli kwa muda mrefu bila mapumzikio (isometric exercises) huongeza presha kwenye mishipa ya damu kwa ghafla.

Hali hii inaweza kusababisha kupasuka kwa mshipa wa damu na kusababisha kiharusi kwa mara nyingine.

Pili ni changamoto za uwiano na uratibu wa mwili (balance & coordination). Udhaifu wa upande mmoja wa mwili (hemiparesis) pamoja me tatizo la mguu kulegea (drop foot) huwafanya waliopona kiharusi kuwa katika hatari kubwa ya kuanguka, kuteguka, au kuvunjika mifupa.

Tatu ni tabia ya kubana pumzi wakati wa mazoezi magumu (Valsalva Maneuver).

Kubana pumzi unaposukuma au kuinua uzito huongeza presha kubwa ndani ya kichwa na kifurani, jambo ambalo ni hatari mno kwa mfumo wa mishipa ya damu uliowahi kuathirika.

Mwisho ni kujilazimisha mazoezi yasiyo na kipi-mo. Kuanza programu za kawaida za gym bila kuzingatia uwezo wa mwili husababisha kulemewa kwa misuli, uchovu uliopitiliza, na msukumo mkubwa kwenye moyo.

Ili kufaidika na mazoezi bila kuhatarisha maisha, wataalamu wanashauri mambo yafuatayo.

Pata kibali cha daktari; Kabla ya kukanyaga gym, muulize Daktari wako wa mfumo wa fahamu (neurologist) au Mtaalamu wa Fiziotherapia (physiotherapist) ili ujue mazoezi yapi ni salama kufanya.


Tumia vifaa sahihi; Anza na mashine za kukaa au resistance bands badala ya vyuma vya mkononi ili kulinda uwiano wa mwili.

Jifunze kupumua vizuri; Usibane pumzi unapotumia nguvu; toa hewa nje unaposukuma uzito na vuta hewa ndani wakati wote wa mazoezi.

Fanya kazi na wataalamu; Mshirikishe Mtaalamu wa Fiziotherapia mwenye uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa fahamu na utangamao (neurological rehabilitation) atakusimamia na atakusaidia kuwa na mpango unaofaa kwa hali yako.

Ili kurejea kwenye afya njema baada ya kiharusi inawezekana, lakini msingi wake mkuu ni nidhamu, uvumilivu, na kufuata muongozo wa wataalamu.

Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob



Bustani ya Sheria



Na Wakili Karim Gabriel Mussa

Hatua ya pili unaponunua ardhi kwa mkataba



BAADA ya kufanya uchunguzi wa hali ya kisheria ya ardhi unayotaka kununua, hatua inayofuata ni kuingia katika hatua ya mkataba (contractual stage).

Hii ni hatua muhimu inayohusisha makubaliano rasmi kati ya mnunuzi na muuzaji kuhusu masharti ya mauziano.

Kwanza, pande hizo zinapaswa kukubaliana kuhusu bei ya ardhi, namna ya malipo, muda wa kulipa na masharti mengine, ikiwemo utaratibu wa kukabidhi mali na kuhamisha umiliki. Ni muhimu makubaliano haya yawekwe kwa maandishi ili kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migogoro baadaye.

Pili, ni muhimu kuandaa mkataba wa mauziano unaoeleza wazi haki na wajibu wa kila upande. Mkataba huo unapaswa kuwa na majina ya wahusika, maelezo yanayotambulisha ardhi inayouzwa, bei, utaratibu wa malipo na masharti mengine yaliyokubaliwa.

Ushauri wa mwanasheria ni muhimu ili kuhakikisha mkataba unaendana na sheria na unalinda maslahi ya pande zote.

Baada ya mkataba kuandaliwa, wahusika wanapaswa kuusoma na kuelewa masharti yake kabla ya kusaini.

Saini za wahusika zinathibitisha makubaliano yao, lakini kusaini mkataba pekee hakuamaanishi kwamba taratibu zote za kisheria za kuhamisha umiliki zimekamiliwa. Kwa hiyo, nyaraka na vibali vingine vinavyotakiwa kisheria vinapaswa pia kushughulikiwa.

Katika mchakato wa kuhamisha umiliki wa ardhi, fomu na nyaraka zinazohitajika hutegemea aina ya haki ya ardhi na mazingira ya mauziano.

Aidha, ikiwa ardhi ni mali ya ndoa, ni muhimu kuchunguza na kupata ridhaa inayotakiwa kisheria ya mwanandoa.

Vivyo hivyo, ikiwa mali inahusiana na mirathi, mamlaka ya msimamizi wa mirathi na taratibu za kisheria zinazohusu mali hiyo zinapaswa kuthibitishwa kabla ya mauziano.

Somo la Kisheria; Usisaini mkataba wa mauziano kwa kutegemea kuaminiana pekee.

Hakikisha masharti yote yameandikwa, nyaraka zimehakikiwa na taratibu za kuhamisha umiliki zimeeleweka. Mkataba mzuri ni hatua muhimu ya kulinda haki zako, lakini ni lazima uendane na matakwa ya sheria.

Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karim-binmussa@gmail.com

Teknolojia ■

Nani anamiliki AI?

Na Mwandishi WETU

AKILI Mnemba, maarufu kwa neno la Kiingereza; Artificial Intelligence yaani kwa kifupi AI, imekuwa moja ya teknolojia zinazobadilisha dunia kwa kasi ya ajabu.

Inatumika kuandika habari, kuchambua takwimu, kutambua magonjwa, kuendesha biashara na hata kufanya kazi ambazo hapo awali zilihitaji wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu.

Lakini wakati dunia ikishangilia mafanikio hayo, swali kubwa linaibuka; Nani hasa anamiliki na kudhibiti AI?

Swali hilo linapata uzito kutokana na onyo la wataalamu wa teknolojia wanaoeleza kuwa binadamu anatengeneza mifumo ya AI ambayo haielewi kikamilifu namna inavyofanya maamuzi.

Kwa mujibu wa tahadhari hiyo, mifumo ya AI inayotengenezwa sasa, au kwa usahihi zaidi inayokuzwa kupitia mafunzo ya kiteknolojia, haiko chini ya udhibiti kamili wa binadamu.

Ingawa binadamu ndiye anaitengeneza, lakini katika matukio kadhaa anashindwa kuelewa kikamilifu kwa nini baadhi ya mifumo hiyo inatoa majibu au kufanya uamuzi fulani. Hata hivyo, hilo halimaanishi kuwa AI ina matamano au nia zinazofanana na za binadamu.

Wataalamu wanaonya kuwa uwezo wa AI unaoongezeka kwa kasi, na katika siku zijazo mifumo hiyo inaweza kufikia hatua ya kusaidia kuboresha teknolojia yake yenyewe, ikiwamo kufanya utafiti ambao kwa sasa unafanywa na binadamu.

Hapa ndipo hatari inapojitokeza.

Ikiwa binadamu atakabidhi majukumu makubwa kwa teknolojia ambayo hawezi kuelewa au kudhibiti kikamilifu, nani atawajibika pale itakapofanya makosa yatakayokuwa na madhara, hasa kwa maisha au mali za watu?

Je, ni kampuni iliyotengeneza mfumo huo, mtaalamu aliyeufundisha, serikali iliyoruhusu matumizi yake au mtu aliyeutumia?

Kwa sasa, kampuni kubwa za teknolojia ndizo zinazomiliki na kuendesha mifumo mingi yenye



uwezo mkubwa wa AI.

Lakini umiliki wa kisheria si sawa na uwezo wa kuelewa na kudhibiti kila matokeo ya teknolojia hiyo.

Ndiyo maana kuna wito wa kampuni hizo kuwa wazi zaidi kwa umma na wataalamu huru, kuimarisha tathmini za usalama na kupunguza kasi ya kutengeneza mifumo yenye uwezo mkubwa hadi usalama wake utakapothibitishwa kwa kiwango kinachokubalika.

Hata hivyo, kupunguza kasi ya maendeleo ya AI kuna mjadala wake. Wapo wanaoamini kuwa teknolojia hiyo inaweza kuleta manufaa makubwa katika afya, elimu, kilimo na uchumi, hivyo kuchelewesha maendeleo yake kunaweza pia kuchelewesha suluhisho muhimu la matatizo katika sekta nyingi.

Kwa Tanzania, mjadala huu haupaswi kuachwa kwa mataifa yenye kampuni kubwa za teknolojia pekee.

Kadiri AI inavyoingia katika benki, hospitali, vyombo vya habari na taasisi za serikali, ndivyo umuhimu wa kuwa na sera, sheria na wataalamu wa kusimamia matumizi yake unavyoongezeka.

Serikali inahitaji kuhakikisha kuwa taarifa za wananchi zinalindwa, maamuzi muhimu yanayosaidiwa na AI yanakaguliwa na binadamu, na taasisi zinazotumia teknolojia hiyo zinawajibika kwa madhara yanayoweza kutokea.

Hatimaye, swali siyo nani anayemiliki AI kibiashara pekee, bali nani mwenye mamlaka ya kudhibiti na nani anayewajibika inapokosea.

■ Uchambuzi



Rais Jakaya Kikwete akisikiliza maelezo toka kwa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe baada ya kupokea mapendekezo ya chama hicho juu ya kuundwa Katiba Mpya, Ikulu jijini Dar es Salaam. Novemba 27, 2011

Freeman Mbowe...

Inatoka Uk. 23

Lakini baadaye alikumbwa na kashfa kubwa za dawa za kulevya, akafungiwa kucheza mwaka 1991 na kuondolewa katika Kombe la Dunia mwaka 1994 baada ya kushindwa vipimo vya dawa zilizopigwa marufuku.

Kashfa hizo ziliathiri sifa yake na umaarufu wake, lakini hazikufuta urathi wake katika soka. Hadi leo, Argentina inaendelea kumuenzi, na Napoli iliupa uwanja wake jina la Maradona alipofariki dunia mwaka 2020. Kuporomoka kwa umaarufu wake hakumaanishi kufutika kwa urathi wake

Ninaposhuhudia mashambulizi na propaganda kali dhidi ya Mbowe mitandaoni, naelewa kuwa umaarufu wake umeathirika. Lakini ninapoitazama Chadema naona alama za Mbowe kila mahali mithili ya njia alikopita konokomo.

Historia ya siasa za upinzani Tanzania haiwezi kuandikwa kwa uaminifu bila mchango wa Mbowe ka-

tika kuibadilisha Chadema kutoka chama kidogo hadi kuwa chama kikuu cha siasa Tanzania chenye mtandao wa kitaifa, viongozi wenye ushawishi na uwezo wa kushindana na CCM tangu 2010.

Warithi wake wana haki ya kubadili mbinu, kukosoa makosa yake na hata kuijenga Chadema kuwa kubwa zaidi. Lakini hawahitaji kumdhalilisha ili kuthibitisha uwezo wao. Taasisi inayojiheshimu haiandiki historia yake kwa kumfuta mmoja wa wajenzi wake wakuu.

Hapo ndipo hoja yangu kuhusu demokrasia inapopata maana. Kama wapigania mabadiliko hawawezi kuvumilia maoni tofauti au hata kasoro za Mbowe, watawezaje kujenga taifa linaloheshimu uhuru wa mawazo ya kila mtu? Hatuwezi kuondoa udikteta kwa kuiga tabia zake.

Badilisheni mbinu za mapambano kama mnavyoonna inafaa, lakini msimlazimishe Mbowe kuwa mtu mwingine, wala msijaribu kufuta historia iliyowafikisha hapo mlipo.

Freeman Mbowe hakukalia tu kiti cha uenyekiti wa Chadema, bali alishiriki kuijenga taasisi iliyokipa kiti hicho uzito, hadhi na ushawishi wa kitaifa.

Mbowe ni kama konokono wa kisiasa. Mwendu wa polepole, subira, tahadhari na ustahimilivu. Anapokabiliwa na hatari, hujificha ndani ya gamba lake. Kila apitapo, huacha alama.

Ana tabia ya mwanzizi; unyumbufu, ustahimilivu na uwezo wa kuinama bila kuvunjika, hata unapokabiliwa na upepo mkali. Mwanzizi huyumba kufuatia upepo, lakini dhoruba inapopita, husimama tena wima.

Mnaweza kukosoa makosa yake, kupinga mbinu zake au hata kuharibu taswira yake mbele ya umma. Lakini hamwezi kufuta kile alichoshiriki kukijenga: Chadema yenyewe. Huo ndio urathi wake usioplingika.

Ansbert Ngurumo ni mwandishi wa habari, mwanafalsafa, mchambuzi wa siasa na mwandishi wa vitabu, mwenye uzoefu wa takribani miaka 30 katika uandishi wa habari, uongozi wa vyombo vya habari na uchambuzi wa masuala ya kisiasa na kijamii. Aliwahi kuwa miongoni mwa viongozi na makada wa Chadema hadi 2019 na mshauri binafsi wa habari na mawasiliano wa chama hicho tangu 2010.

Waziri Chongolo afagilia mafanikio ya ‘dhababu ya kijani’

Na Mwandishi WETTU

ZAO la parachichi linazidi kuvutia wakulima na wawekezaji nchini Tanzania kutokana na nafasi yake katika kuongeza kipato, kutengeneza ajira na kuingiza fedha za kigeni kupitia mauzo katika masoko ya kimataifa.

Zao hilo, linaloitwa “dhahabu ya kijani”, limekuwa miongoni mwa mazao yanayopewa msukumo na serikali ili kupanua uzalishaji na kuwawezesha wakulima kunufaika na mahitaji yanayoongezeka.

Waziri wa Kilimo, Daniel Chongolo (pichani), amehimiza uwekezaji katika zao hilo, akieleza kwamba mapato yake yameongezeka zaidi ya maradufu ndani ya miaka mitano.

Kwa takwimu alizoeleza, mapato yalipanda kutoka dola za Marekani milioni 44.2 mwaka 2020/2021 hadi dola milioni 97.2 mwaka 2025/2026. Hilo ni ongezeko la dola milioni 53, sawa na takribani asilimia 120.

Ukuaji huo unaonyesha nafasi ya parachichi katika biashara ya kilimo na kwamba msukumo zaidi utamaanisha mazao na fedha zaidi.

Kwa mkulima, manufaa yake yanatokana na kuuza matunda yenye ubora unaokidhi mahitaji ya wanunuzi. Mafanikio yanahitaji miche bora, huduma sahihi shambani, uvunaji kwa wakati na utunzaji unaozuia matunda kuharibika.

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), linasema parachichi linakuwa chanzo muhimu cha kipato, ajira, uwekezaji na mapato ya mauzo nje nchini Tanzania.

Fursa zake zinaenea zaidi ya mashambani. Uzalishaji unahitaji wafanyakazi, huku ukusanyaji, upangaji wa madaraja, ufungashaji na usafirishaji vikifungua milango ya biashara kwa



vijana, wanawake na watoa huduma.

Chongolo anawaasa wakulima na wawekezaji kwamba usindikaji wa parachichi unaweza kuongeza thamani kwa kutengeneza mafuta ya parachichi, hatua inayopanua matumizi ya zao hilo na nafasi za uwekezaji wa viwanda.

Waziri huyo wa kilimo amesema kuwa serikali imeeleza dhamira ya kuimarisha uzalishaji, kuongeza thamani na kupanua masoko ya ndani na nje.

Hata hivyo, FAO inaonya kwamba uwezo huo unahitaji kushughulikia changamoto za miche, usimamizi wa mashamba, uvunaji, utunzaji baada ya kuvuna na upatikanaji wa masoko.

Kwa hiyo, kupanua mashamba kunapaswa kwenda sambamba na taarifa za bei, mikataba inayoeleweka na miundombinu ya kuhifadhi matunda.

Thamani ya “dhahabu ya kijani” itaonekana zaidi pale ongezeko la mauzo litakapoboresha maisha ya wakulima, kuimarisha biashara za vijijini na kuifanya Tanzania kuwa msambazaji wa kuaminika wa parachichi bora katika masoko yenye ushindani mkubwa duniani.

■ Kutoka Jimboni

Chinyele ni sauti inayobeba ajenda za ustawi Dodoma Mjini



Paschal Chinyele akihojiwa na mwandishi wetu, Hellen Ngoromera jijini Dodoma. (Picha na Mpigapicha Wetu).

Na Hellen NGOROMERA

KAZI kubwa na inayopaswa kuwa ya kutukuka ya mbunge, ni kuwakilisha matamano ya wananchi kwa serikali ili kuchochea ustawi wa jamii.

Mbunge anapofanya kazi zake kwa ufanisi, weledi na kuwasilisha serikalini – kupitia Bunge, nini wananchi wanataka kuona yakitekelezwa na serikali, anakuwa anatimiza wajibu na haki ipasavyo.

Wapo wabunge wanaofanya kazi zao kuhakikisha waliomtuma, wanafaidi uwepo wake bungeni, na wananchi hawana wasiwasi wa “kuangushwa” naye.

Imani ya wananchi wengi ni kwamba ubunge wenye maana huonekana pale mahitaji ya wananchi yanapogeuzwa kuwa hoja zinazotaka majibu na hatua kutoka serikalini.

Katika kuzingatia hayo, Mbunge wa Dodoma Mjini, Paschal Inyasi Chinyele, amekuwa miongoni mwa wabunge “wanaojielewa” akionekana kupambana kuhakikisha matamano ya wananchi anayejengea hoja ili serikali kuchukua hatua.

Michango yake bungeni inaonyesha juhudi za kuweka mbele masuala yanayogusa maisha ya wapigakura wake, anazungumzia changamoto za maji, barabara, elimu ya ufundi na fursa za uzalishaji.

Katika Jiji la Dodoma linalokua kwa kasi, maendeleo hayawezi kupimwa kwa majengo marefu na makubwa pekee, bali yanapaswa kuonekana pia katika upatikanaji wa huduma kwa wakazi wote, wakiwame wale wanaoishi pembezoni mwa jiji hilo, ambalo ni makao makuu ya nchi.

Imani ya Chinyele ni katika kutimiza majukumu yake ni kuona kwamba barabara nzuri zikiunganisha wananchi na masoko, shule, hospitali na shughuli za kiuchumi.

Katika huduma ya maji, Chinyele ameuliza amswali na kujenga hoja bungeni kuhusu kukamilishwa kwa miradi ya Nzuguni, Nala na Zuzu, akieleza changamoto za wakazi na vituo vya afya.

Huu ni mfano wa uwakilishi unaovuka mipaka ya ukumbi wa Bunge.

Chinyele amehoji pia kuanza kwa mafunzo katika Dodoma Polytechnic College iliyopo Lugala, Mbalawala. Swali hilo linaunganisha uwekezaji wa serikali na matarajio ya vijana kupata ujuzi unaoweza kuwasaidia kujenga maisha yao.

Aidha, ameitaka serikali kueleza utekelezaji wa mipango ya kongani za viwanda Nala na Mpunguzi. Kusukuma hoja za uzalishaji kunaweka mbele matarajio ya ajira, masoko na kuongeza thamani ya mazao.

Juhudi hizi zinastahili kutambuliwa kwani zinatoa mfano unaoweza kuigwa wa mbunge anayebeba mahitaji ya wananchi na kuyafikisha kwa wenye mamlaka kwa ajili ya utekelezaji.

Sauti inayounguruma zaidi

Dodoma Mjini inahitaji sauti inayouliza, inayofuatilia na inayosisitiza matokeo; na juhudi za Chinyele hazikinzani na msingi wa matarajio hayo.

Katika mahojiano maalum na Gazeti la Pambazuko wiki iliyopita ofisini kwake, Chinyele anasema hamu ya kushughulikia kero zinazowakabili wakazi wa jimbo analoongoza ndiyo jambo lililomsikuma kugombea lengo la kugombea ubunge.

Kutoka Jimboni ■

Chinyele ni sauti...

Inatoka Uk. 30

“Wakati nagombea ubunge mwaka jana, tayari nilifanya utafiti nikagundua changamoto sita zinazowakabili watu wa jimbo ambazo ni maji, barabara kubwa na za mtaani, uhafifu wa huduma za elimu, afya na migogoro ya ardhi na huduma hafifu za umeme,” anasema Chinyele.

Akieleza kuhusu kero ya maji, anabainisha kuwa jiografia ya jimbo hilo ina sura mbili ambazo ni mjini na vijijini.

Anasema wakati Tarafa ya Dodoma Mjini ipo mjini, Tarafa ya Zuzu, yenye kata saba (Chigongwe, Mbalawala, Nala, Zuzu, Mbabala, Matumburu na Mpunguzi) ziko katika mazingira ya kijijini ambako shughuli kubwa za uchumi ni kilimo na ufugaji.

“Ukienda leo Chigongwe hakuna huduma ya umeme, wala maji hakuna na inafikia hatua wananchi wanachangia maji na ng’ombe...”

“Watu wanategemea kilimo na ufugaji wa ng’ombe kwa hiyo ukienda utaona kwamba hapa hauko mjini,” amesema Chinyele.

Anaasema hali hiyo imemsukuma kuanzisha harakati kadhaa za kuhakikisha wananchi hao wanapata huduma ya maji.

Mbunge huyo anasema kwa kiasi kikubwa amekuwa akitumia fedha za Mfuko wa Jimbo kutatua kero hiyo.

Hata hivyo, anasema fedha hizo zilikuwa chache kwani kutokana na kugawanywa kwa jimbo hilo ilibidi hata fedha hizo, kiasi cha Shilingi milioni 92, nazo zigawanywe baina ya majimbo hayo.

Mbunge huyo anasema alitumia kiasi kikubwa cha fedha hizo kuchimba visima katika Kata ya Chang’ombe na katika Kata ya Zuzu katika Mtaa wa Chididimo na hadi sasa miradi hiyo inaendelea kufanya kazi.

Serikali igawe Jiji la Dodoma

Chinyele anasema miongoni mwa mambo ambayo ana kiu nayo yaweze kutimia ni serikali kuliga wa Jiji la Dodoma ili liwe na halmashauri mbili.

“Jiji hili linastahili kuwa na halmashauri zaidi ya mbili, lakini kwa sababu tunafahamu uwezo wa serikali ni mdogo kwa sasa, nashauri serikali igawe halmashauri mara mbili.

“Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikae katika jiografia ya Jimbo la Mtumba na Manispaa ya Mazengo ikae katika jiografia ya Jimbo la Dodoma Mjini,” anasema Mbunge Chinyele.

Anatoa mfano wa akieleza kuwa Jiji la Dodoma lina ukubwa wa kilometa za mraba 2,607 wakati Mkoa na Dar es salaam una kilometa za mraba 1,590 na kubainisha kuwa kilometa 1,590 za Dar es Salaam ndizo zilizo-gawanywa katika halmashauri tano.

“Ninachosema ni kwamba kwa kuwa serikali inapeleka fedha kwa wananchi kupitia halmashauri, wakazi wa Dodoma mjini yenye Kata 41 kuendelea kuhudumiwa na jiji lenye halmashauri moja ni kuwatwisha wananchi mzigo...”

“Dodoma imekuwa halmashauri tangu ikiwa manispaa moja watu walikuwa wachache, lakini sasa watu wamekuwa wengi kwa sababu imekuwa makao makuu ya nchi, lakini halmashauri bado ni moja...”

“Tukipata halmashauri nyingine serikali itakuwa imeongeza bajeti kwa ajili ya watu wachache. Hili ni pendekezo langu ambalo nilianza nalo wakati wa kampeni, lakini pia ni pendekezo langu sasa na wakati mwingine wowote ikiwa halitatekelezeka,” ameongeza.

Barabara mpya

Mbunge huyo ameishauri serikali kujenga barabara kutoka Dodoma hadi Mbeya kupitia Makongolosi ili kurahisisha usafiri na usafirishajina pia kuimarisha uchumi wa nchi.

“Njia hii ninayoipendekeza itafupisha sana safari kutoka Dodoma kwenda Mbeya. Ujenzi wa barabara hiyo una maslahi ya kimkoa, kijimbo na kitaifa...”

“Hivi sasa Dodoma inaunganishwa na Mbeya kupitia Iringa kwa umbali za zaidi yab kilometa 600, lakini njia ninayoipendekeza ikifunguliwa, itakuwa na urefu wa kilometa 340 pekee,” amesema Chinyele.

Amesema hali hiyo itaboresha ulinzi na usalama kwani wanyama watazaliana na uchumi wa nchi utapaa lakini kubwa zaidi mizigo kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam itafika Zambia na DRC kwa haraka kuliko ilivyo sasa.

Pamoja na matamano yake na kubeba maono ya wananchi anaowaongoza, Mbunge Chinyele, tayari uwajibikaji wake umedhihiri kwa kufanya ziara za mara kwa mara kwa wapigakura na kuchukua maoni yao, huku baadhi ya sehemu zikianza kuonja “nguvu zake” kupigania jimbo kwa maendeleo.

■ Barua za Wasomaji



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

Katiba Mpya inapaswa kupiganiwa na wote

Mhariri,

WIMBO wa Katiba Mpya unapaswa kuimbwa na kila Mtanzania mwenye utashi na akili timamu.

Hivi ni nani asiyejua umuhimu wa Katiba katika kuongoza nchi?

Kuna msemu unaosema Katiba imara huzaa serikali imara, hivyo hivyo kwa Katiba dhaifu huzaa serikali dhaifu.

Nawashangaa sana baadhi ya wanasiasa wanaobeza umuhimu wa Katiba Mpya na huenda mbali zaidi kwa kusema eti 'Katiba haiteti chakula nyumbani' huwa najiuliza hivi wanafanya kusudi au kweli hawajui umuhimu wa Katiba Mpya.

Tunataka Katiba itakayoleta manufaa kwa taifa, Katiba itakayowajibisha viongozi dhidi ya rushwa na ufisadi, Katiba itakayompa mamlaka mwananchi ya kuchagua kiongozi anayemtaka na kura yake kuheshimiwa.

Katiba inapaswa kusimamia rasilimali za taifa na kuweka mgawanyo sawa wa keki ya taifa, Katiba itakayoleta usawa wa kijinsia, uhuru wa maoni na demokrasia ya kweli itakayoakisi mfumo wa vyama vingi.

**Hassan Juma,
Bariadi, Simiyu**

Kimara tunateseka kwa foleni

Mhariri,

BARABARA ya Kimara imekuwa kero kwa wakazi kutokana na ujenzi unaoendelea, ambapo umekuwa ukisababisha msongamano mkubwa wa magari kila siku jioni.

Kilio hiki cha muda mrefu kimekuwa sugu na mateso kwa wakazi na watumiaji wa barabara hii ya Morogoro, kiukweli tunateseka sana na kadhia hii kila ifikapo jioni.

Tunaomba mamlaka husika watu-saidie wakazi wa Kimara na Mbezi kutuondolea mateso haya, pia barabara ya Kimara hadi Ubungo iishe mapema ili kusiwe na foleni.

**Samuel John,
Kimara Mwisho,
Dar es Salaam.**

Kongole TMA, vyombo vya habari

Mhariri,

KUPITIA gazeti lako pendwa la Pambazuko, ninai-pongeza Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa (TMA) pamoja na vyombo vya habari kwa kutoa tahadhari na taarifa juu ya ujio wa mvua kubwa za El-Nino zinazotarajiwa kuanza kunyesha mwezi huu Oktoba hadi Desemba.

Wananchi wamepata taarifa za kutosha kuhusu mvua hizi.

Lakini pamoja na hilo, mvua iliyonyesha hivi karibuni katika eneo la Kariakoo, imeonyesha kwa kiwango kikubwa bado miundombinu yetu haipo ta-

yari kwa kupokea mvua hizi.

Hilo linajidhihirisha kutokana na mvua hiyo kunyesha ndani ya dakika 45 tu lakini ilivyonyesha kila mahali maji yalijaa hadi kwenye barabara.

Nitoe mwito kwa mamlaka husika kwamba mvua iliyonyesha Kariakoo imetuma salamu kwetu sisi wananchi pamoja na viongozi kufanya kazi ya ziada kwa kuendelea kufanya usafi kwenye miundombinu ya kupitisha maji (mitaro).

**Janeth David,
Tabata Sanene,
Dar es Salaam.**

Habari katika Picha ■

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), akiwa kwenye Dua ya 40 ya Marehemu Maalim Hafidh Ameir Hassan, aliyekuwa mume wa Rais Samia Suluhu Hassan, iliyofanyika katika Msikiti Mkuu wa Kizimkazi, Kusini Unguja, juzi. (Picha na Ikulu).



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Regina Qwaray akikabidhi vitimwendo kwa watoto wenye mahitaji maalum, ikiwa ni hatua ya kusaidia wazazi hasa akina mama waliokuwa wanalazimika kuwabeba mgogoni. Hafla hiyo ilifanyika mkoani humo mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu).



Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba, akizungumza na wawekezaji wa kampuni za uchimbaji, uchenjuaaji na uuzaji wa madini kwenye soko la dunia na benki za Gold World Council, Stone X na Kampuni ya Geita Gold Refinery (GGR) inayomilikiwa na kuongozwa na mwekezaji, Sarah Masasi katika ukumbi wa mikutano wa Hotel ya Hayyat, London, Uingereza juzi. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).



Mufti Ismail Musa Menk (katikati) kutoka Zimbabwe akisoma Dua kwenye hitma ya 40 ya Marehemu Maalim Hafidh Ameir Hassan aliyekuwa mume wa Rais Samia Suluhu Hassan, iliyofanyika katika Msikiti Mkuu wa Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja juzi. (Picha na Ikulu).



Kamera ya Pambazuko jana iliwakuta baadhi ya wakazi wa Tabata Kinyerezi, Kifuru, Dar es Salaam wakichota maji ambayo siyo salama katika Bonde la Kifuru kutokana na kuwepo shida ya kupatikana maji safi na salama.

■ **Makala**

Wanaume wanateseka kimyakimya

Zaidi ya wanaume 8,200 walifanyiwa ukatili wa kijinsia mwaka 2025, huku wataalamu wakieleza kuwa hofu ya kudharauliwa na jamii inawafanya wengi kushindwa kueleza mateso wanayopitia.



Na Hellen NGOROMERA

WANAWAKE, kwa miaka mingi wamekuwa wakitajwa kuwa waathirika wakubwa wa ukatili wa kijinsia na kusababisha serikali na taasisi mbalimbali kuanzisha kampeni zinazolenga kumlinda dhidi ya ukatili huo.

Lakini kampeni iliyoendeshwa na Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima (pichani), imeonyesha upande mwingine wa shilingi ambako wanaume nao wamebainika kuwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Kampeni hiyo ya Dkt. Gwajima imeonyesha kuwa ukatili dhidi ya wanaume ni moja ya changamoto zinazohitaji kupewa uzito zaidi katika jamii, kwani watu wengi walijitokeza kueleza jinsi wanaume wanavyoteseka kimyakimya katika jamii.

Uchambuzi wa Pambazuko umebaini pia

kuwa hilo siyo suala la nadharia tu kwani hata Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonyesha kuwa wanaume 8,228 walikuwa miongoni mwa wahanga wa ukatili wa kijinsia walioripotiwa kwa Jeshi la Polisi mwaka jana.

Idadi hiyo ni sawa na asilimia 27.3 ya wahanga wote 30,127 walioripotiwa mwaka huo, ikionyesha kuwa wanaume pia wanakabiliwa na vitendo vya ukatili, ingawa mjadala wa kijamii mara nyingi umejikita zaidi katika mateso wanayopitia wanawake.

Mwaka uliotangulia hali ilikuwa mbaya zaidi kwani wanaume walioripotiwa kupitia ukatili ni 11,965, wengi zaidi kuliko mwaka 2025.

Pamoja na kupungua kwa idadi ya matukio yalioripotiwa, wataalamu wa masuala ya saikolojia na mahusiano wanaeleza kuwa wanaume wengi bado wanashindwa kuzungumzia changamoto wanazokabiliana nazo katika ndoa kutokana na mitazamo ya kijamii inayowatarajia kuwa wavumilivu, jasiri na wasiolia.

Hali hiyo imeibua mjadala mpya kuhusu namna jamii inavyoshughulikia ukatili wa majumbani, hasa katika kipindi ambacho kume kuwa na taarifa za mauaji yanayohusisha wanandoa na wapenzi katika maeneo mbalimbali nchini.

Takwimu zinasema nini?

Mbali na takwimu za Jeshi la Polisi, utafiti kuhusu ukatili wa wenza zinaonyesha kuwa wanaume na wanawake wanaweza kukumbana na aina tofauti za unyanyasaji katika uhusiano.

Katika utafiti mmoja uliowahusisha wanau-me 1,113 na wanawake 226, asilimia 34.8 ya wanaume na asilimia 35.8 ya wanawake waliripoti kufanyiwa angalau aina moja ya ukatili kutoka kwa wenza wao katika miezi 12 iliyotangulia.

Ukatili uliohusika na matukio hayo ulihusisha vitendo vya kimwili, kingono na kisaikolojia.

Inaendelea Uk. 35

Wanaume wanateseka

Inatoka Uk. 34

Matokeo hayo yanaonyesha umuhimu wa kuchunguza ukatili wa wenza kwa kuzingatia uzoefu wa jinsia zote mbili, badala ya kudhani kuwa mhanga lazima awe mwanamke.

Utafiti mwingine uliowahusisha watu 2,299, wakiwamo wanaume 744, ulichunguza uzoefu wa ukatili wa wenza na namna wahanga wana-vyowashirikisha wengine kuhusu mateso wan-ayopitia.

Aidha, utafiti wa mwaka 2024 uliolenga vija-na na watoto ulibaini kuwa asilimia 9.3 ya vijana wa kiume waliowahi kuwa na wenza waliripoti kufanyiwa ukatili wa kihisia na wenza wao kati-ka maisha yao.

Kwa upande wa Zanzibar, asilimia 18.5 ya vi-jana wa kiume waliripoti kufanyiwa ukatili wa kihisia kutoka vyanzo mbalimbali katika mai-sha yao.

Takwimu nyingine za mwaka 2024 zinaone-sha asilimia 36.3 katika kiashiria cha wanaume waliopata huduma na kuripoti ukatili wa kim-wili, huku asilimia 5.9 ikihusishwa na ukatili wa kingono.

Hata hivyo, asilimia hizo zinahusu makundi maalumu yaliyofanyiwa utafiti au kupata hudu-ma, hivyo haziwezi kutumika kuwakilisha wa-naume wote nchini.

Wanaume waogopa kusema

Akizungumza na Pambazuko, mtaalamu wa saikolojia na uhusiano, Charles Kalungu, anase-ma changamoto zinazowakabili wanaume ni nyingi kuliko zinavyoonekana katika mijadala ya kawaida ya jamii.

Kwa mujibu wake, tatizo kubwa si ukosefu wa changamoto hizo, bali mazingira yanayowafan-ya wanaume waone aibu au waogope kuzieleza.

“Wanaume wana kero nyingi zaidi ya zinazo-fahamika. Shida ni kwamba hazipewi kipaum-bele...”

“Kutokana na mifumo na desturi zilizopo, wakati mwingine mwanaume anakosa nafasi ya kusikilizwa,” anasema Kalungu.



Siyo ajabu kuwa katika kampeni yake isiyo rasmi, Dkt. Gwajima amepata mrejesho mkub-wa kutoka kwa wanaume.

Hii inaonyesha haja ya kufanyika kwa kamp-eni rasmi ya kuibua ukatili wa jinsia wanaofa-nyiwa wanaume. Kalungu anaeleza kuwa jamii imejenga taswira ya mwanaume kuwa mtu mwenye nguvu, jasiri na anayeweza kustahimili changamoto bila kuomba msaada.

Kwa sababu hiyo, mwanaume anapojitoke-za kueleza kuwa ananyanyaswa au anaumizwa kihisia, anaweza kuonekana dhaifu au asiye na uwezo wa kuongoza familia.

Kalungu anasema mtazamo huo unawafan-ya baadhi ya wanaume kubaki na matatizo yao kwa muda mrefu, badala ya kutafuta ushauri au msaada wa kitaalamu.

Anasema kukosekana kwa nafasi salama za kuzungumza kunaweza kuongeza msongo wa mawazo, migogoro na kushindwa kutatua ma-tatizo kwa njia zinazofaa.

Hata hivyo, wataalamu wanasisitiza kuwa changamoto za kihisia au ukatili anaoupitia mtu haziwezi kutumika kuhalalisha kumdhuru au kumuua mwenza wake.

Mauaji ya wenza yazua maswali

Katika siku za karibuni, taarifa za mauaji yanayohusisha wanandoa na wapenzi zime-ongeza wasiwasi kuhusu namna migogoro ya kimahusiano inavyoshughulikiwa.

Miongoni mwa matukio yaliyozua mjadala ni lile la Bunju, Dar es Salaam, ambako mwa-namke aliuawa kwa kupigwa risasi katika tukio ambalo mumewe alitajwa kuwa mtuhumiwa.

Inaendelea Uk. 36

Wanaume wanateseka

Inatoka Uk. 35

Kalungu anasema matukio kama hayo yanaonesha umuhimu wa kutambua mapema dalili za migogoro mikubwa katika mahusiano na kuhakikisha wahusika wanapata msaada kabla hali haijawa mbaya zaidi.

Kwa mtazamo wake, baadhi ya watu hukaa na maumivu ya kihisia na malalamiko kwa muda mrefu bila kupata njia sahihi ya kuyashughulikia.

Wataalamu wanaeleza kuwa mauaji ya wenza yanaweza kuhusishwa na mambo mbalimbali, yakiwamo tabia za udhibiti, vitisho, wivu, migogoro ya mali na historia ya ukatili.

Waziri Gwajima afungua mjadala

Hali ya wanaume kunyanyaswa kimyakimya katika jamii imeibuliwa na mjadala ulianzishwa na Waziri Dkt. Gwajima kuhusu changamoto zinazowakabili wanaume katika ndoa na familia kupitia mtandao wa TikTok.

Mjadala huo uliwapa wanaume nafasi ya kueleza uzoefu wao kuhusu migogoro ya ndoa, mahusiano, changamoto za kiuchumi, malezi ya watoto na namna wanavyohisi kutendewa na wenza wao.

Katika kipindi kilichodumu kwa saa nne na dakika 26, takwimu zilizotolewa zilionyesha kuwa mjadala huo ulifikia watazamaji 108,900, ulipata maoni 10,300 na alama za kupendezwa 270,500, huku wafuasi wapya 2,200 wakijitokeza katika akaunti hiyo ya Waziri Gwajima.

Baadhi ya waliochangia walieleza kuwa wanaume wana matatizo mengi ambayo mara nyingi hawapati nafasi ya kuyazungumza.

Mchangiaji mmoja alisema; “Wanaume hatusemi, ila tupo kwenye changamoto kubwa sana.”

Mwingine aliyejitambulisha kama Sondak-achoji, alimshukuru Waziri Gwajima kwa kutoa nafasi hiyo, akieleza kuwa wanaume wanahitaji kusikilizwa kama makundi mengine katika jamii.

Mjadala huo, ambao pia uliwashirikisha baadhi ya viongozi wa dini, uliibua hoja kuhusu umuhimu wa mawasiliano katika ndoa,

kuheshimiana, uaminifu na uwajibikaji wa wanandoa.

Wanaume yahimizwa

Kalungu amepongeza hatua ya Waziri Gwajima kuanzisha majadiliano hayo, akisema inaweza kusaidia kupunguza unyanyapaa unaowakabili wanaume wanaotaka kueleza changamoto zao.

Anasema wanaume wanapopewa nafasi ya kuzungumza, wengine wanaopitia matatizo yanayofanana hupata ujasiri wa kutafuta msaada.

“Unapowasiliza wanaume watano, saba au 10 wakieleza changamoto zao, wengine wanaowasiliza wanagundua kuwa si wao pekee wanaopitia hali hizo,” anasema.

Anaongeza kuwa hata wanawake wanaofuatilia mjadala hiyo wanaweza kupata fursa ya kuelewa changamoto zinazowakabili wenza wao na namna ya kuboresha mawasiliano katika familia.

Kwa mujibu wake, mjadala hiyo haipaswi kuwa ya muda mfupi, bali iendelezwe kupitia makongamano, semina na programu za elimu kwa vijana wanaojiandaa kuingia katika ndoa.

“Nadhani utaratibu huu unapaswa kuwa endelevu. Yafanyike makongamano mengi zaidi ya wanaume ili kuwasaidia vijana ambao watakuwa baba wa familia zijazo kujitambua na kuelewa wajibu wao mapema,” anasema.

Jamii inapaswa kufanya nini?

Wakati mjadala kuhusu ukatili dhidi ya wanaume ukiendelea, wataalamu wanaona umuhimu wa kujenga mfumo unaotambua na kushughulikia ukatili dhidi ya mtu yeyote bila kujali jinsia.


Hii inahusisha kuimarisha huduma za ushauri nasaha, kuongeza uelewa kuhusu ukatili wa kisaikolojia na kuhakikisha madawati ya jinsia na watoto yanakuwa sehemu salama kwa wanaume na wanawake wanaohitaji msaada.

Pia kuna umuhimu wa kuwahamasisha wanandoa kutafuta ushauri mapema, badala ya kusebiri migogoro ifikie hatua ya vitisho, vipigo au mauaji.

Kwa upande mwingine, wataalamu wanaonya kuwa usuluhishi wa ndoa haupaswi kupewa kipaumbele kuliko usalama wa mtu ambaye tayari anakabiliwa na vitisho au ukatili.

Harambee... ■

Bati/ Mtu, Mtu Bati HATUCHOKI!



Mawasiliano:

0754 742 423

Askofu Benson K Bagonza


Changia kupitia

NMB A/C NO 31910046325

ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT

CRDB A/C NO 0150764151900

UWAKILI PROJECT ELCT KAD



Wanandoa kataeni ukatili

HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Nakukaribisha tena kwenye wiki nyingine ili kupeana elimu na maarifa ya maisha.

Wiki hii nitazungumza namna misingi ya ndoa na uhusiano inavyoweza kujengwa bila kuathiriwa na ukatili.

Ukatili kwenye ndoa au uhusiano siyo kosa la bahati mbaya, bali ni uhalifu na suluhisho la matatizo haya halianzi kwenye vyombo vya sheria bali nyumbani.

Ndoa nyingi na uhusiano katika maisha ya sasa vinatawaliwa na changamoto nyingi ambazo kwa kiasi kikubwa husababisha athari kubwa ikiwemo wenza kudhuriana na wengine kufikia hatua ya kutoana uhai.

Jambo la msingi la kuzingatia kwenye uhusiano ni kuwa na mawasiliano yasiyo na kelele. Mara nyingi kutokuelewana katika ndoa au uhusiano kunatokana na wenza kutozungumza kwa utulivu bali hutumia hasira jambo ambalo huzua mtafaruku.

Ili kuepuka mikwaruzano inawapasa kutenga muda wa kuzungumza kwa utulivu hoja zenu mbalimbali zinazowahusu.

Mke ana haki ya kusema anachohisi kwa mwenzake bila kuogopa kupigwa hali pia mwanamume naye ana haki ya kusikilizwa bila kudharauliwa. Ndoa bila mazungumzo ni bomu.

Jingine ni uchumi huru. Pesa ni mingoni mwa vyanzo vikubwa vya ukatili. Mwanamke asiye na kipato chake mara nyingi huvumilia manyanyaso kwa sababu ya kukusa mahali pa kwenda jambo ambalo halifai.

Suluhisho la jambo hili ni wanawake kuwezeshwa kiuchumi na wanaume kuacha ubinafsi wa kipato. Pesa ya familia ni ya familia na sio silaha.

Sheria isimame. Mara nyingi unapotokea ugomvi kwenye ndoa wazee ndio huamua kwa kiasi kikubwa kwa kumtaka mwanamke kuvumilia na mwisho wa siku humweka mkosewa katika wakati mgumu.

Kikubwa kinachopaswa kufanywa hapa ni sheria kuchukua mkondo wake.

Ikitokea kesi moja ikahukumiwa hadhara-ni kwa kumkuta mtuhumiwa na kosa, itaokoa ndoa 100 na zaidi.

Malezi na dini ni vitu vya msingi vinavyopaswa kutiliwa mkazo. Ikitokea watoto wanaona baba anampiga mama yao nao wataiga tabia hiyo.

Vyombo vya dini makanisa, misikitini na vingine vikemee ukatili badala ya kuuficha kwa kisingizio cha ndoa.

Ndoa ni hifadhi, siyo jela, ikitokea unapitia ukatili wa kutukanwa au mwingine, tafuta msaada mapema kwani ukifumbiwa macho unaweza kuleta madhara mengine makubwa.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■



Jihan alivyotikisa na vazi la taifa Miss Grand

JIHAN Dimack ameiwakilisha Tanzania kwenye Miss Grand International 2026 kupitia vazi la taifa (National Costume) lenye kuonyesha utajiri wa utamaduni na urithi wa Tanzania.

Mrembo huyo amevalia mchangan-yiko wa asili ya Tanzania ikiwemo mavazi ya kimasai, wanyama pori na majengo ya zamani yanayopatikana Visiwani Zanzibar.

Jihan ambaye alikuwa mwakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Miss Grand International, alivuta hisia za wen-

gi na kubamba mitandaoni kutokana na ubunifu wa vazi hilo.

Vazi hilo ambalo lilibuniwa na mbuni-fu maarufu kutoka nchini Thailand, Akarach Phusanaphong, lilikuwa limebeba maana nzito za kiutamaduni na kijiografia za Tanzania.

Ujumbe wa vazi hilo, ulikuwa ukiwakilisha urithi wa waswahili na Visiwa vya Zanzibar, mbuga za wanyama na utajiri wa madini ya kipekee duniani ya Tanzania.

■ **Burudani****Fahamu historia ya Jihan****Ni mshindi wa dunia wa Miss Grand International****Na Mwandishi WETU**

MREMBO Jihan Dimack, ameandika historia kwa kuwa Mtanzania wa kwanza kutwaa Taji Kuu la Miss Gand International tangu mashindano hayo yali poanzishwa mwaka 2013.

Jihan aliibuka kuwa mshindi wa taji hilo juzi Oktoba 10, 2026, katika fainali ya mashindano hayo iliyofanyika jijini Bangkok – Thailand.

Jihan mwenye uzoefu mkubwa katika ulimwengu wa mitindo na mashindano ya urembo, awali alitwaa taji la Miss la Miss Grand Tanzania 2026, akiwakili-

sha Mkoa wa Mwanza.

Ushindi huo ndiyo ulio-mpa nafasi ya kuiwakilisha Tanzania katika Miss Grand International 2026, Thailand.

Mrembo huyo mwenye asili ya Kitanzania na Lebanon, kwa sasa amekuwa akifanya kazi nchini China katika maeneo ya modeling, mauzo na live commerce.

Alianza rasmi kujihusisha na mitindo akiwa na umri wa miaka 17, anaeleza kuwa uzoefu wa kuishi katika tamaduni tofauti umemjengea mtazamo mpana kuhusu utofauti wa watu na tamaduni duniani.

Marioo alivyotwaa tuzo za Afrimma**Na Mwandishi WETU**

MSANII wa Bongo Flewa, Om-ary Ally Mwanga maarufu Marioo, ameshinda Tuzo ya Msanii wa Bora wa Kiume Afrika Mashariki katika tuzo za AFRIMMA mwaka 2026, zilizo-fanyika Septemba 12, 2026 jijini Dallas, Texas nchini Marekani.

Marioo alichuana na wasanii mbalimbali akiwemo Diamond Platnumz, Juma Jux, Barnaba (wote kutoka Tanzania), Bien kutoka Kenya, Eddy Kenzo na Joshua Baraka kutoka Uganda.

Mbali na ushindi huo, Marioo pia alipata nafasi ya kupanda jukwaani na kutumbuiza kwenye tamasha hilo la Afrimma Music Fest.

Michezo Kimataifa ■



Barcelona wanatesa La liga, Madrid Mmh!

Na John MARWA

WAKATI msimu wa kandanda wa 2026/27 kwa Ligi mbalimbali duniani ukizidi kuchanganya, huko Hispania, Timu ya Barcelona, hawacheki na kima, wananyonga tu, wakati wapinzani wao, Real Madrid bado hayajakaa sawa.

Ikiwa kila timu imeshuka dimbani mara nane, tayari Barcelona chini ya mtaalamu Hansi Flick, basi lao limechanganya kwa kushinda michezo yote nane, ushindi asilimia mia moja, wakifunga mabao 34 na kuruhusu 7.

Wastani wa kufunga ni mabao 4.25 kwa mechi huku kuruhusu ikiwa ni 0.9 kwa mchezo, na sasa ikiwa nafasi ya kwanza kileleni pointi 24.

Nafasi ya pili wapo Atletico Madrid, michezo nane, ushindi michezo sita, sare moja na kupoteza mmoja, mabao ya kufunga 18, wastani kufunga mabao 2.25, huku wakiruhusu mabao 8, wastani wa bao moja kila mchezo, pointi 19 kibindoni, tofauti ya alama 5 dhidi ya kinara Barcelona.

Wakati huohuo, Real Madrid ya Jose Mourinho ikiwa nafasi ya tatu, pointi 18, ushindi michezo 6 na kupoteza miwili.

Mabao yao ya kufunga ni 18, wastani wa mabao 2.37, huku kuruhusu ni bao moja kila mchezo. bado mzani unayumba pale Santiago Bernabeu, licha ya vita kuwa mbichi lakini unit zinasoma.

Barcelona wanaonekana kukamilika maeneo yote ya uwanja, wanacheza kwa swaga, wanafunga wanavyotaka, hii ni ishara nzuri kwa Hansi Flick na vijana wake msimu huu japo bado ndo alfajiri jua linachomoza, japo biashara ni asubuhi jioni mahesabu.

Madrid wameshindwa kutamba kwa Atletico Madrid ya Diego Simion ambapo walipoteza kwa mabao 2-1, huku Real Bets nao wakiwanyoosha kwa bao 1-0.

Je, ni nini hasa ambacho Mourinho atakifanya na Los Blancos kumdhibiti Hansi Flick na Diego Simion? Ni jioni ya 2026/27 itakayotoa majawabu msimu huu.



Wamebonda na kunyonga!



Na John MARWA

HATIMAYE Timu ya Simba imewabonda wapinzani wao wa jadi, Klabu ya Yanga na kuziba mwanya wa uteja wa muda mrefu.

Kifupi, Simba wameibonda vibaya sana Yanga, baada ya kuonyesha mchezo mzuri na “mkubwa” katika mchezo uliochezwa jana, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Siku ya dabi hiyo ilisubiriwa sana na hatimaye jana, Oktoba 10, 2026, historia ya ku-

kataa uteja ikazimwa.

Miaka mitatu na nusu iliyopita, Simba walikuwa dhofulihali mbele ya Yanga kwenye mitanange ya Ligi Kuu Soka Tanzania Bara, lakini jana wameonyesha ubabe wa kabumbu uwanjani.

Simba walimchakaza mpinzani wao kibabe, wakamtia mateso makali na kupata mabao 2-1.

Ni mchezo ambao kila mpenzi wa soka, na hata mashabiki wanaoelewa soka, wanakiri kwamba ulikuwa mzuri, huku Simba akionekana kutawala vipindi vyote viwili, licha ya Yanga kuongoza kwa bao la mapema – dakika ya tano tu.

Kocha Steve Barker wa Simba aliiandaa timu yake vyema na huenda kuhimiza uvumillivu na kusukuma presha hata baada ya kuwa wamefungwa bao 0-1 hadi kipindi cha kwanza kinamalizika.

Goli la Yanga lilipatikana baada ya makosa ya Neo Maema, ambayo yakaipa Yanga uongozi kupitia Peter Shalulile.

Hata hivyo, kipindi cha pili, kiungo mtunduizi, Neo Maema akafuta makosa yake kipindi cha pili kwa kuweka mzani sawa dakika ya 67.

Wakati Yanga bado wanajikagua kama wako salama, Elie Mpanzu akatukumbusha ya Ronaldo De Lima 2006 kwenye michuano ya Kombe la Dunia dhidi ya Ghana. Aliwezesha timu yake kubitika kidedea licha ya kubanwa na wapinzani wao.

Watasema nini wana Simba zaidi ya shukrani kwa Mola wao, ikiwa kila kitu katika mchezo huo ni wao, kila takwimu ni zao. Mungu wao amewakumbuka na amejibu maombi yao, furaha sasa imerejea kwa miamba ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo.

Kufuatia matokeo hayo, Simba hakuchukua tu pointi tatu, bali amerejesha, heshima na utu wake, pointi 21 michezo 7.